SUPA JACKPOT
TZS. 1,144,172,464
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Ndugu** Bilionea Msuya aangua kilio kortini

UKURASA 3




UKURASA 11

# Nipashe

Jumamosi Agosti 19, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581407

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



Askofu Methodius Kilaini

Katibu Mkuu wa TEC, Dk. Charles Kitima

Rais wa TEC, Askofu Gervas Nyaisonga

SAKATA LA BANDARI

# TEC yatoa tamko zito

- **Askofu** Munga asema ni la kinabii, BAKWATA yatoa neno... *Ukurasa 2*

UKURASA WA 4



## NDUGAI AHADHARISHA UAGIZAJI NJE MAFUTA YA KULA

SPIKA Mstaafu wa Bunge, Job Ndugai, ameshauri serikali kuangalia suala la uagizaji...

## Ajali gari la Polisi, Kirikuu yaua watu 10

UKURASA 2



UKURASA 3

Wakili Boniface Mwabukusi (wa pili kulia), akisubiri kuingia kwenye gari lake baada ya kuachiwa kwa dhamana katika Kituo Kikuu cha Polisi Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Slaa, Mwabukusi watema cheche baada ya kuachiwa kwa dhamana

**MICHEZO** GAMONDI: NAHITAJI MABAO MENGI CAF UK.24 **KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao cha Baraza la Mawaziri, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Ajali gari la polisi, Kirikuu yaua watu 10

**Na Waandishi Wetu**

WATU 10 akiwamo askari wa Jeshi la Polisi mwenye namba G. 8813 Koplo Denis Mamkwe (38) wa Chuo cha Polisi Moshi (CCP), wamefariki dunia katika ajali iliyotokea eneo la Datch Konner, wilayani Siha mkoani Kilimanjaro.

Ajali hiyo ilitokea jana baada ya gari ndogo, maarufu kama Kirikuu, kuyumba kutokana na kupata hitalafu katika gurudumu la kulia na kugongana uso kwa uso na lori la polisi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, alisema gari la polisi lilikuwa likienda Kambi ya Pori na Kirikuu iliyokuwa na wafanyabiashara wakiwa na mizigo ikitokea Sanya Juu ilikuwa ikienda Ngarenaro sokoni.

Alisema tukio hilo lilitokea majira ya saa 6:00 mchana katika eneo la Kilingi karibu na makao makuu ya wilaya ya Siha.

"Awali, dereva wa gari hilo (Kirikuu) alikamatwa kwa kosa la kupakia abiria kinyume cha sheria na taratibu na kutozwa faini na baada ya hapo, alipofika katika kituo kinachofuata alipakia abiria wengine. Gari la polisi lilikuwa likiendeshwa na G. 8813 Denis lilipasuka tairi na kusababisha ajali hiyo,

Aliwataja waliofariki dunia, mbali na Mamkwe, kuwa ni Sarah Minja (45), Gloria Lema (39) mkazi wa Lawate, Adela Kanyorota (24) mkazi wa Sanya Juu na Mary Nkya (45), mkazi wa Machame Lambo.

Wengine ni Matilda Mwabukusi (52) mkazi wa Kitahemwa Manio, Siha, Getruda Muro mkazi wa Boma na John Mushi (25) mkazi wa Machame Narumu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali Maalumu ya Magonjwa Ambukizi Kibongoto, Dk. Leonard Subi, alisema wamepokea miili 10 iliyotokana na ajali hiyo, wanawake wakiwa sita na wanaume wanne.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Kilimanjaro ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Nurdin Babu, ikiwa hospitalini hapo, ilitoa pole na kutoa rai kwa wananchi kuendelea kufuata sheria za usalama barabarani.

"Tumepoteza maisha ya watu ambao jamii, familia na taifa linawategemea. Madereva hakikisheni hamtumii vileo na tumieni udereva wa kujihami ili unapokutana na tatizo uweze kuwa salama," alisema Babu.

Majeruhi Neema Mboye ambaye amebaki peke yake baada ya ajali hiyo, akiwa Hospitali ya Wilaya ya Siha, alisema alichoona ni gari la Jeshi la Polisi likiwa mwendo kasi na kuivamia Kirikuu.

"Dereva wa Kirikuu awali alipigwa faini hivyo, alikosa amani, gari la polisi likiwa linatokea likiwa limewasha taa, dereva wa Kirikuu akawaza anasimamishwa tena ndiyo muda huo huo nikaona matairi ya gari la polisi yananyanyukia kwenye Kirikuu," alisema.

**Imeandaliwa na Mary Mosha na Anjela Mhando (SIHA).**

# TEC yatoa tamko sakata la bandari

**Na Restuta James**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), limetoa tamko kuhusu mkataba wa ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kati ya Tanzania na Dubai (IGA) katika uendeshaji na uboredhaji wa bandari za Bahari na maziwa nchini.

Aidha, katika tamko hilo lililojumisha maaskofu 37 wa majimbo yote Tanzania, baraza hilo limeishauri serikali iwasikilize wananchi na kumwomba Rais Samia Suluhu Hassan kusitisha wasilisho la ridhio la IGA kwa serikali ya Dubai lililopitishwa bungeni, Juni 10, mwaka huu. Pia wameshauri Bunge lifute ridhio hilo.

Tamko la TEC lenye kurasa nane, lililotiwa saini na Rais wake, Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga na Katibu Mkuu wake, Padre Dk. Charles Kitima, limesema 'Sauti ya watu ni sauti ya Mungu' na kwamba kuwasikiliza na kufanya uamuzi kadiri wananchi wanavyotaka ni kuiletea heshima serikali.

Viongozi hao walisema mijadala, maoni na mapendekezo ya wananchi wengi yanaonyesha wanapinga makubaliano ya mkataba huo kati ya serikali ya Tanzania na Dubai.

Walisema wananchi wana shauku ya kuona uendeshaji wa bandari unafanywa na Watanzania baada ya uwekezaji uliofanywa na serikali katika miundombinu ya bandari, reli na bandari kavu.

"Hali kadhalika, tumegundua mapungufu yetu ya uendeshaji wa bandari...tunao uwezo wa kuendelea kujizatiti kurekebisha mapungufu yanayojitokeza wakati njia za kiuchumi zikibaki mikononi mwetu.

"Kwa vile wananchi walio wengi hawataki uwekezaji wenye masharti mabovu kama haya (IGA) katika bandari zetu na kwa kuwa serikali inawajibika kwa wananchi, lazima viongozi wasikilize sauti ya watu, kwani sauti yao ni sauti ya Mungu."

"Ni vyema, ni busara na ni hekima serikali kuwasikiliza wananchi maana kutowasikiliza ni kujiletea matatizo makubwa zaidi siku za usoni kwani wananchi hawa hawa watavitaka vizazi vijavyo kuondokana na unyonyaji huu," ilisema sehemu ya tamko hilo.

Tamko hilo liliongeza kuwa maaskofu hao wametoa tamko baada ya kusikiliza maoni ya wananchi, serikali na wadau wengine wa maendeleo; wakasali na kutafakari yaliyozungumzwa tangu makubaliano ya IGA yawekwe hadharani.

"Tukisukumwa na dhamiri iliyo na lengo la kulinda rasilimali, mshikamano, amani, uhuru na umoja wa kitaifa, tunathubutu kusema kuwa baada ya miaka 63 ya uhuru wa nchi hii, wananchi hawajapenda kuiachia bandari ya Dar es Salaam apewe mwekezaji mmoja aiendeshe," lilifafanua tamko hilo.

**MAPENDEKEZO MAHSUSI**

Kutokana na msimamo huo, TEC imeshauri kwamba badala ya serikali kuzikodisha bandari kwa kampuni ya DP World, iendelee kujenga uwezo wa kitaifa kwa sekta za umma na binafsi nchini kwa kuingia ubia na kampuni zilizobobea kwenye teknolojia kwa mikataba yenye tija kwa taifa.

"Utaratibu wa serikali kuweka wawekezaji kutoka nje tu katika njia kuu za uchumi umekosesha uendelevu wa vitega uchumi vyetu hasa pale wawekezaji wanapoondoka...bandari ikiwa ni moja ya njia kuu na ya asili inayotuwezesha kufanya biashara kubwa na mataifa mbalimbali, ni lazima iendelee kuwa biashara ya Watanzania wenyewe na ibaki mikononi mwetu hata kama tunaingia ubia wenye tija," lilifafanua tamko hilo.

**IBARA ZINAZOLALAMIKIWA**

Kwa mujibu wa tamko hilo, TEC ilitaja ibara tisa zinazoibana zaidi Tanzania ambazo ni ya 2 (1) inayoweka utaratibu wa kuendeleza, kuboresha na kuendesha bandari za bahari, maziwa na maeneo maalumu ya uwekezaji.

Ibara zingine ni ya 4 inayoilazimisha Tanzania kuiarifu Dubai pale kunapotokea fursa ya uwekezaji kwenye bandari, ya 5 inayoipa DP World haki ya kuendeleza, kusimamia na kuendesha miradi ya bandari na ya 6 inayoitaka Tanzania kuipatia kampuni hiyo vivutio vya kutekeleza miradi yake.

Ibara zingine ni ile ya 7, 8, 10, 23 na 24 ambazo pamoja na mambo mengine, zinaeleza namna ya kuvunja mkataba, haki za mwekezaji na usiri wa mikataba ya utekelezaji kati ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) na DP World.

**BAKWATA, DK. MUNGA**

Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), kupitia Katibu Mkuu wake, Shekhe Nuhu Mruma, lilisema maaskofu hao wametumia nafasi yao kutoa maoni na kwamba ni wajibu wa serikali kutoa ufafanuzi wa hoja walizozitoa.

Mruma alisema ni muhimu kuwa na uvumilivu na kuipa serikali nafasi ya kujibu tamko na maoni ya wananchi kwa kuwa bado elimu zaidi kuhusu faida za uwekezaji kwenye bandari inahitajika. Askofu Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (K.K.K.T), Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Dk. Stephen Munga, aliipongeza TEC kwa kufanya kazi ya kitume vizuri kwa kuainisha mambo yote ya msingi na athari za kuendelea na IGA.

"Wametoa sauti yao ya kinabii na sauti hii isiposikilizwa ni kweli madhara yake yataonekana kwa vizazi vijavyo. Ningeomba serikali isikilize," alisema.

HABARI KITAIFA

# Ndugu wa Bilionea Msuya aangua kilio mahakamani

**Na Grace Gurisha**

NDUGU wa marehemu Aneth Msuya, ameangua kilio ndani ya mahakama, wakati shahidi namba 17, Sajini John Mwambusye (55) aliyepata mafunzo ya ukaguzi wa matukio kutoka kwa Shirika la Upelelezi la Marekani (FBI), akieleza jinsi alivyokuta mwili wa marehemu ukiwa mtupu na damu nyingi zikiwa zimetapakaa chini.

Kesi hiyo ya mauji namba 103 ya mwaka 2018 inamkabili mke wa Erasto Msuya, maarufu kama Bilionea Msuya, Miriam Mrita, na mfanyabiashara Revocatus Muyella, wanaotuhumiwa kumuua, Aneth, nyumbani kwake Kigamboni, Dar es Salaam Mei 25, 2016.

Mwambusye alieleza hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi wake kwa kueleza jinsi alivyofika eneo la tukio na kukusanya vielelezo vitatu kisu, chupi ya rangi ya zambarau na filimbi yenye rangi ya silva.

Mtaalamu wa Uchunguzi wa Sayansi ya Jinai, alipata mafunzo yake kutoka kwa FBI na Uturuki na kutunukiwa cheti cha ukaguzi wa matukio na cheti cha ukusanyaji wa vielelezo.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Paul Kimweri, Mwambusye alidai kuwa Mei 26, 2016 majira ya saa 1:00 asubuhi, alikuwa ofisini kwake Kituo cha Polisi Chang'ombe na Mkuu wa Upelelezi wa makosa ya Jinai wa Mkoa (RCO) wa Kipolisi wa Temeke, Richard Mchomvu, alimfuata na kumweleza kuwa waende eneo la Kibada, Kigamboni kukagua eneo la tukio la mauaji.

"Nilifanya maandalizi nikachukua sanduku la vifaa kwa ajili ya kukagua eneo. Tulipofika picha ya kwanza niliyoiona ni utepe wa Jeshi la Polisi ulikuwa umefungwa kwenye geti la kuingia ndani kwenye nyumba ya marehemu," alidai Mwambusye.

Aliendelea kudai kuwa nje ya utepe huo kulikuwa na watu wengi ambao wamezunguka nyumba na waliingia ndani ya geti yeye na Mchovu na baada ya kuingia, walikutana na Mkuu wa Upelelezi wa Kigamboni, Richard Mwasemba na askari Fredrick Mwigike.

"Walitueleza kwamba hapo ndani kuna tukio la mauaji. Baada ya hapo nikaanza kukagua kuanzia mlango wa sebuleni. Nilichokiona huo mlango ulikuwa umevunjwa na niliendelea kukagua chumba kimoja hadi kingine, niligundua kulikuwa na vipande vya matofali.

" Wakati naendelea kufanya ukaguzi, niliingia kwenye chumba ambacho nilikuta mwili wa marehemu umelala chini hauna nguo (uchi) na damu nyingi zikiwa sakafuni na baadhi ya nguo na nyaraka mbalimbali hazikuwa katika mpangilio nzuri," alidai. Mwambusye

Alidai kuwa mwili huo ukiwa tupu, aliukuta ukiwa na jeraha la kitu chenye ncha kali, pembeni ya mwili aliona kisu kikiwa na damu na pembeni ya kitanda aliona nguo ya ndani yenye rangi ya zambarau ikiwa imejiviringa na filimbi yenye rangi ya 'silver'.

Shahidi alipomaliza tu kuzungumza hayo, ndugu wa marehemu Aneth (mwanamke) ambaye hakufahamika jina lake, aliangua kilio ndani ya ukumbi wa wazi wa mahakama huku akigumia kwa uchungu akitikisa kichwa na kusema kwa sauti ya chini kwamba hawezi kuendelea kusikiliza.

Ndugu huyo ambaye alianza kulia kwa sauti ya chini, baadaye kushindwa kuvumilia na kuangulia kilio kikali ambacho kilifanya ukumbi wa mahakama uwe kimya kwa muda, alisema anaumia sana kwa tukio hilo.

Hali hiyo ambayo alishindwa kujizuia, ilisababisha askari wa Jeshi la Magereza amfuate na kumweleza kwamba aende nje ya chumba cha mahakama, hali ambayo ilimfanya alie kwa nguvu huku akitolewa ukumbini.

Baada ya kutolewa nje, Shahidi Mwambusye aliendelea kudai kuwa alichukua kisu kwa sababu mwili wa marehemu ulikuwa na jeraha la ncha kali kwa ajili ya uchunguzi wake wa kisayansi wa vinasaba.

Pia alidai kuwa alichukua chupi kwa ajili ya kutaka kujua endapo marehemu Anneth aliingiliwa kingono na kwa kielelezo cha filimbi alikichukuwa kama aliomba msaada kwa kupulizwa filimbi. Alidai baada ya kukusanya na kuviweka alama vielelezo, alivipeleka Kituo cha Polisi Kigamboni.

Shahidi huyo alidai kuwa Agosti 28, 2016 Mchovu alimtuma akachukue vielelezo hivyo Kituo cha Polisi Kigamboni na kuvipelekea Kituo cha Polisi Chang'ombe na kumkabidhi WP (polisi wa kike) Elentruda ambaye alijaza fomu ya polisi namba 180.

Pia alidai kuwa Mchovu aliwapa maelekezo yeye na Elentruda kuvipeleka vielelezo hivyo Makao Makuu ya Uchunguzi wa Sayansi Jinai kwa sababu WP Elentruda ndiye alikuwa amebeba vielelezo hivyo yeye ndiye aliyevikabidhi.

Akijibu maswali ya Wakili Peter Kibatala, shahidi alidai kuwa hakumueleza Jaji kama ufunguo wa mlango ambao alikuwa amevihifadhi vielelezo hivyo alikuwa nao yeye.

Pia alidai yeye na WP Elentruda wakati wanakabidhiana vielelezo hawakujaza fomu ya polisi namba 145 na pia alidai kuwa wakati anamkabidhi WP mwaka vielelezo katika Kituo cha Polisi Kigamboni hawakumwambia jaji kama kuna sehemu waliandikishiana.



Mabaki ya gari Suzuki Carry yenye namba za usajili T292 DEU baada ya kugongana na lori la polisi aina ya Ashok Leyland namba PT 4081 katika eneo la Dachi, Sanya Juu jana na kusababisha vifo vya watu 10 na majeruhi mmoja. Habari Uk. 2 **PICHA: MARY MOSHA**

# Slaa, Mwabukusi watema cheche baada ya kuachiwa kwa dhamana

**Na Waandishi Wetu**

MWANASIASA Mkongwe na mwanadiplomasia, Balozi Dk. Willibrod Slaa, Wakili Boniface Mwabukusi na Mdude Nyagali, wameachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti huku wakifunguka kuwa hawatarudi nyuma.

Dk. Slaa ambaye alikuwa mahabusu kwa siku tano katika Kituo cha Polisi Oysterbay mkoani Dar es Salaam, alikuwa wa kwanza kupewa dhamana jana asubuhi.

Baadaye jioni, Wakili Mwabukusi na mwanaharakati Mpaluka Nyagali, maarufu kama Mdude, waliokuwa wakishikiliwa kituo cha polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma za uhaini, nao wakaachiwa kwa dhamana baada ya kubadilishiwa mashtaka ya uhaini na kuwa ya uchochezi.

Wawili hao wameachiwa baada ya kukidhi vigezo vya dhamana ambavyo ni kuwa na wadhamini wawili kila mmoja wenye mali zisizohamishika zenye thamani isiyopungua Sh. milioni 10.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, akiwa nyumbani kwake, Mbweni mkoani Dar es Salaam, muda mfupi baada ya kuachiwa, Dk. Slaa alisema hatarudi nyuma katika kutetea rasilimali za taifa hata kama atapatwa na mabaya.

Balozi Slaa ambaye alikuwa anakabiliwa na tuhuma za uhaini na sasa haijabainishwa mashtaka yake mapya, alisema yuko tayari kuhukumiwa kwa kutetea maslahi ya wananchi.

"Kama Bunge tulilolichagua haliyasemei haya, lazima sisi wengine tujitose kuyasema haya na hili kama litaitwa tena uchochezi waliite tu. Kama Bunge haliyasemei na sisi Mungu alitujalia tukasoma, tunayaelewa, tutaendelea kusema. Kama kuwekwa ndani, tuwekwe tu, ndiyo maana jela zipo.

"Sitarudi nyuma kutetea rasilimali za taifa, hasa rasilimali bandari ambayo imezungumziwa kwa miezi kadhaa sasa," alisema.

Akisimulia alivyokamatwa, Dk. Slaa alisema akiwa nyumbani kwake akiwasiliana na Watanzania kupitia Club House, ghafla ilipigwa hodi na walipoingia watu hao, walijitambulisha kuwa ni askari kisha kumkamata.

Alisema wakati watu hao wakimkamata, hawakumweleza kosa lake na baada ya muda mfupi, alirudi nao nyumbani kwake na kupekuliwa.

"Hapa tulipokaa ndipo nilipokamatiwa siku ya tarehe 13 na nilikamatwa wakati ninazungumza na sauti ya Watanzania, nilishtukia mlango unagongwa kwa nguvu sana.

"Waliokuwa wanagonga walikuwa hata hawana uvumilivu, wanataka kuvunja geti, mimi sikuwa na haraka kwa vile nipo nyumbani, wakanilazimisha nipande kwenye gari yao nikaenda nao.

"Sikujua tunakwenda kufanya nini? tulipiga round (kuzunguka) tukarudi tena hapa, wakasema wanataka kufanya upekuzi. Mungu aliruhusu na kwa kuwa nilikuwa kwenye sauti ya watanzania, niliwajulisha kuwa wamekuja kunikamata," alisema.

Kuhusu mashitaka yanayomkabili, alisema kwa kuwa hajapandishwa mahakamani hana uhakika, ingawa mwanzo aliambiwa ana makosa ya uhaini.

Wakili Mwabukusi na Mdude, wakizungumza na waandishi mara baada ya kuachiwa, waliwashukuru Watanzania ambao walikuwa wanapiga kelele kwa muda wote wa siku sita ambazo walikuwa wanashikiliwa.

Wakili Mwabukusi alisema kitendo cha kuwekwa ndani hakijawayumbisha na hivyo, wanakusudia kutoa mwelekeo mpya wa kuendelea kupigania haki za watanzania kwa kupinga mikataba ambayo haina tija kwa taifa.

"Kwanza tulikuwa tunashikiliwa kimakosa lakini niwaambie tu Watanzania kwamba walichokuwa wanakusudia ilikuwa ni kutuua kwa sababu adhabu ya uhaini ni kunyongwa, hiki walichotufanyia hakituyumbishi hata kidogo," alisema Wakili Mwabukusi.

Alisema wanakusudia kuonana na Balozi Slaa ili kujadiliana namna sahihi ya kuendeleza gurudumu la kutetea rasilimali za taifa hasa Bandari ya Dar es Salaam.

Mdude kwa upande wake alisema kitendo cha kuwaweka ndani kimewaongezea zaidi nguvu ya kuwatetea watanzania kwa maelezo kuwa yeye kuwekwa huko ni kitu cha kawaida.

"Niwaambie tu kwamba, mimi vituo vya polisi ni chumbani kwangu na magereza ni sebuleni kwangu, kwa hiyo walichokifanya hapa ni kunitekenya tu," alisema Mdude.

Wakili aliyekuwa anawatetea, Philip Mwakilima, alisema wateja wake waliachiwa baada ya kupata wadhamini wawili kila mmoja wenye mali zenye thamani isiyopungua Sh. milioni 10 ambao wanatoka kwenye kata wanazoishi.

Alisema wateja wake walipewa dhamana baada ya kubadilishiwa makosa ya uhaini na kuwa ya uchochezi na wanatakiwa kuripoti Kituo cha Polisi Jumatatu.

Wakili Mwabukusi na Mdude walikamatwa mkoani Morogoro, Agosti 12, mwaka huu, usiku kisha wakasafirishwa kupelekwa mkoani Mbeya ambako baadaye waliunganishwa na Balozi Dk. Slaa ambaye alikamatwa jijini Dar es Salaam.

**Imeandaliwa na Enock Charles (DAR) na Mwandishi Wetu (Mbeya).**



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Mlezi wa chama hicho Mkoa wa Lindi, Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda akitoa maelekezo baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa madarasa mapya ya mradi wa Boost katika Shule ya Msingi Kijiji cha Tunduru, wilayani Nachingwea juzi. Kushoto ni Mkuu wa wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndugai atoa tahadhari uagizaji nje mafuta ya kula

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

SPIKA Mstaafu wa Bunge, Job Ndugai, ameshauri serikali kuangalia suala la uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi kwa kuwa linashusha uzalishaji wa alizeti nchini kutokana na kuwapo kwa bei isiyo na tija kwa mkulima.

Akizungumza jana wilayani hapa kwenye uzinduzi wa kiwanda cha kusindika mafuta ya alizeti kinachomilikiwa na Quickstep Investment Limited kilichofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Ndugai alisema bei ya alizeti na mafuta ya kula kuanzia mwaka jana imekuwa si ya kuvutia kwa wakulima kutokana na kikwazo cha soko na bei katika mnyororo wa thamani.

"Bei inapokuwa ndogo mkulima anapata hasara na analazimika kulima mazao mengine badala ya alizeti. Mwaka jana serikali iliweka kama azimio hivi la kuhakikisha tunajitosheleza kwa mafuta ya kula nchini kwa kutenga mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu kwa kuanzia kama mikoa maalum ya kilimo cha alizeti," alisema.

Alisema jambo hilo lilipokewa vizuri na wakulima na alizeti ilizalishwa kwa wingi sana lakini ilikumbana na uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi ambao ulishusha bei na kuwavunja moyo wakulima na mwaka huu uzalishaji umepungua.

"Inawezekana uzalishaji kurudi tena na kuvuka pale tulipokuwa endapo bei itakuwa nzuri. Suala la kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ni la kuliangalia sana, rafiki zetu wa TBS (Shirika la Viwango Tanzania) na wengine wote.

"Hebu jaribuni kujifunga mkanda angalau kwa miaka miwili au mitatu tutafika mahali ambapo tunaweza kabisa kujitegemea kwa mafuta ya kula na zaidi, ardhi tunayo ya kutosha," alisema na kusisitiza kuwa bei ikiwa nzuri kila mkulima atakwenda shambani kuzalisha alizeti.

Ndugai alisema suala lingine ambalo serikali inapaswa kuzingatia ni mbegu za alizeti ambazo zinahimili vikwazo na kutoa mafuta mengi.

"Mbegu nyingi zilizopo unapata mbegu bora. Mwaka juzi kama ulilima ukarudia tena mwaka jana, mwaka huu ukilima hupati kitu. Ni mbegu zile ambazo uzalishaji wake unapungua mwaka hadi mwaka.

"Kilimo chetu sasa ni lazima uende dukani kila mwaka ukanunue mbegu. Kwa hiyo mbegu ni ghali hazipatikani na zingine ni feki. Mkulima anaingia gharama kubwa, eneo hili la mbegu ni muhimu kuangaliwa sana," alisema.

Hata hivyo, alisema bidhaa ya mashudu yanayotokana na alizeti bado hayatumiki ipasavyo nchini na yamekuwa yakinunuliwa na kupelekwa Kenya.

Mgeni rasmi katika ufunguzi wa kiwanda hicho, Mkurungenzi wa Maendeleo ya Viwanda kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Lugano Wilson, alisema mafuta ya kula yanayoagizwa kutoka nje ya nchi ni asilimia 60.

Dk. Wilson alisema serikali itaendelea kuwawekea mazingira mazuri ya kufanyia kazi na kuwasaidia kutafuta soko la ndani na nje la mafuta ya alizeti yanayozalishwa nchini.

Alisema ili kufanikiwa katika kuanzisha viwanda vingi zaidi hasa maeneo ya vijijini nishati ya umeme inahitajika kufanikisha lengo hilo.

Awali, akitoa salamu za UNIDO, Gerald Runyoro alisema shirika hilo limefadhili mashine hizo za kusafisha mafuta ya alizeti baada ya kuridhishwa na andiko la watu waliojitokeza kuomba.

Runyora alisema mashine hizo zimetengenezwa nchini na Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Dodoma kwa thamani ya mashine moja Sh. milioni 17.9, hivyo kwa mashine tatu ni Sh. milioni 53.7.

Aliongeza kuwa mashine hizo mbili zimekwenda kwa wananchi wilaya ya Kongwa na moja itakwenda Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) Mkoa wa Dodoma na itakuwa ikitumika kutoa mafunzo kwa wananchi wengine ili kuongeza thamani ya mafuta yanayotengenezwa nchini na kupata soko la nje ya nchi.

# TRA yaitupia zigo manispaa sakata kufungwa baa maarufu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imekanusha kuhusika na kufungiwa kwa baa ya The Cask iliyoko katika Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza na huku ikiitupia mzigo Manispaa kuwa ndiyo inahusika.

TRA katika kujiweka kando na Sakata hilo, imesema suala hilo liko chini ya halmashauri na kwamba haina taarifa zozoto juu ya madai yaliyoibuliwa kuhusu baa hiyo.

Mamlaka hiyo imetoa kauli hiyo kupitia taarifa yake kutokana na agizo la kufungwa kwa baa hiyo na biashara zake zote lililotolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela akieleza kuwa inaendesha biashara bila kuwa na leseni.

Nakala ya TRA mtandaoni iliutaka umma na wahusika wote kuhakikisha wanawasiliana na mamlaka husika juu ya jambo hilo na haihusiki kwa lolote na ilipotafutwa na Nipashe kufafanua juu ya suala hilo, walisema liko chini ya uongozi wa halmashauri husika.

Nipashe ilimtafuta Meneja wa baa hiyo, Edward Mgaya ili kupata ufafanuzi juu tatizo hilo na kusema walipokea barua ya kufunga shughuli zao na hawajakaa na mkurugenzi ili kupata ufafanuzi juu ya sababu ya kuwafungia biashara zao.

Alisema walikuwa wakifanya shughuli zao kwa muda mrefu kwa kufuata sheria na taratibu zote za biashara lakini Agosti 16, mwaka huu, walipokea barua ikiwataka kufunga shughuli zao kutokana na kutokulipa kodi kwa zaidi ya miaka miwili.

Pia alisema licha ya baa yao kufungwa, wamepokea taarifa ya TRA kutokuhusika na suala hilo ambalo kimsingi ni jukumu lao la kujua biashara ipi inatakiwa kulipa kodi na ipi haijalipia kwa muda gani na mpaka sasa bado hawajafunguliwa shughuli zao.

"Tunatarajia kuzungumza na mkurugenzi leo (jana) baada ya kufungiwa ili tupate ufafanuzi wa jambo hilo na hapo tutakuwa na ufafanuzi wa kina juu ya sisi kufungiwa maana hata sisi hatujaelewa bado," alisema Mgaya

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, Kiomoni Kibamba, Agosti 16, mwaka huu, aliwapa barua The Cask yenye kumbukumbu na 45/200/01/33 kuwataka kufunga shughuli zao kwa kile alichokieleza kuwa hawajalipa kodi kwa zaidi ya miaka miwili.

Pamoja na mambo mengine, alisema baa hiyo imekiuka Sheria ya Leseni za Biashara Sura 208 kifungu cha 3(1) kifungu kidogo 'a' na 'b'kwa kuendesha biashara ya vileo,Shisha na chakula bila kuwa na leseni hivyo kuwataka wafunge mpaka watakapotimiza matakwa ya kisheria.

Akizungumza baada ya kufungia baa hiyo, Kibamba alisema baa hiyo inajihusisha na biashara ya matangazo ambayo hakuyataja huku akisema hatua hiyo ni kinyume cha sheria.

"Ukisoma Sheria ya Biashara ya vileo kifungu namba 86 ni marufuku kuchanganya biashara za matangazo tofauti na leseni ambayo umepewa. Pia hana leseni ya biashara kwa miaka miwili. Pia kuna shida nyingine za kimapato sasa tumeona kwamba asitishe shughuli zake kuanzia kesho(juzi) na alitakiwa afunge leo lakini ili vyakula vyake visiharibike atafunga kesho," alieleza Kibamba

Hivi karibuni baadhi ya wanachama wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHANDEMA) walionekana katika baa hiyo wakiendelea na burudani zao wakiwa na bango lenye tangazo la The Cask Bar huku yakipita maneno kwa njia ya kielekitroniki yakisema kuwa 'Okoa Bandari Zetu' hali inayohusishwa na kufungiwa kwa baa hiyo.

## HABARI KITAIFA

# Familia inayodai miradhi yaomba msaada

**Na Abdallah Bakari,**
MTWARA

FAMILIA ya ndugu wa marehemu wanaodai fedha za mirathi mkoani Mtwara imeiomba serikali kutoa tamko kuhusu hatima ya fedha inazodai baada ya ubadhirifu kufanywa na baadhi ya watumishi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mtwara.

Katika mahojiano maalum na mwandishi wa habari, msimamizi wa mirathi jalada namba tano la mwaka 2021 katika Mahakama ya Mwanzo Mahuta Wilaya ya Tandahimba, Hamisi Sabuni, alisema bado serikali haijatoa hatima ya wanaodai fedha hizo.

"Mirathi ninayoifuatilia ni ya marehemu Athuman Sadi Ibrahimu aliyefariki dunia Februari 5, 2021. huyu marehemu alikuwa mwalimu wa shule ya msingi na alistaafu mwaka 2017 na mwaka 2018 alilipwa mafao yake.

"Baada ya kulipwa mafao yake alifungua akaunti ya muda maalum Namba 71010031571 benki ya NMB Tawi la Tandahimba. Pia alikuwa na akaunti ya akiba namba 71008000855 katika benki hiyo hiyo," alisema.

Alisema kwa mujibu wa Athuman wakati wa uhai wake akaunti ya muda maalum ilitarajia kufika ukomo wake Julai Mosi, mwaka huu, kwamba zaidi ya Sh. milioni 70 ziliwekwa.

"Nilikwenda benki kujua salio halisi hadi siku akaunti inafungwa, nikaambiwa akaunti hiyo ilifungwa na niende mahakamani. Nilipofika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara wakaniambia hawana taarifa kuhusu mirathi hiyo.

"Awali nilisotea miezi saba (Januari hadi Julai) mwaka huu kuapishwa ili niwe msimamizi baada ya aliyekuwa msimamizi kuondolewa na wanafamilia na kunichagua mimi.

"Wakati ninafuatilia suala la kuapishwa walionyesha wanalifahamu jarada langu ila leo wanasema hawalifahamu, hivyo sijaelewa kuna nini. Ninaiomba serikali iingilie kati suala hili ili tujue hatima ya fedha hizo" alisema Sabuni.

Mtoto wa tatu wa marehemu, Farida Sadi, alisema baba yake ameacha watoto sita na mjane ambao kwa sasa wanaishi kwa shida kutokana na kukosa fedha za kujikimu na kwamba fedha za mirathi zilikuwa tumaini kwao.

"Siku zote tulikuwa tunaishi kwa matumaini ipo siku moja tabu zitaisha, lakini kwa sasa hatujui kinachoendelea, ila tunaelekea kukata tamaa," alisema.

Mtendaji wa Mahakama hiyo, Richard Mbambe, amewataka wananchi wanaodai mirathi kupitia mahakama hiyo kuendelea kusubiri hatima ya sakata hilo.

"Suala lolote likifika mwisho litafahamika. Suala si bado linaendelea, hivyo hatuwezi kuongelea suala ambalo bado linaendelea," alisema Mbambe.

Awali, gazeti hili liliibua uwapo wa ubadhilifu wa fedha kiasi cha Sh. milioni 695.5 katika kipindi cha mwaka 2020/22.

Mtendaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Leornad Magacha, katika mahojiano ya awali yaliyofanyika Julai, 13, mwaka huu, alisema: "Wananchi wasiwe na wasiwasi wowote, haki zao za mirathi hazitapotea."

Hivi karibuni, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa TAKUKURU Mkoa wa Mtwara, iliomba kibali kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), kwa ajili ya kuwafikisha mahakamani watumishi watatu wa kada ya uhasibu wa Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara, kwa tuhuma za ubadhirifu wa Sh. milioni 234.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari, Jumatano ya wiki hii ofisini kwake, Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mtwara, Jumbe Makoba, alisema tayari upelelezi wa shauri hilo umekamilika na kwamba kinachosubiriwa kwa sasa ni kibali cha DPP.

"TAKUKURU tulipata taarifa kwamba, kuna fedha za mirathi zilizokuwa zinawahusu wanufaika wa mirathi wa ndugu zao waliofariki, lakini zililetwa Mahakama Kuu wakawa wamezifanyia ubadhirifu."

"Ni kweli tumeshachunguza na kukamilisha uchunguzi wa fedha Sh. milioni 234 ambazo zimefujwa na majalada yake tayari tumeyapeleka kwa DPP kwa ajili ya kuomba kibali kuwafikisha mahakamani wahusika," alisema Makoba.

Alisema wanaendelea kukamilisha uchunguzi mwingine wa fedha zaidi ya Sh. milioni 460 zinazohusiana na tuhuma hizo na wakikamilisha watazifikisha kwa DPP kuombea kibali.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Gracian Makota (kushoto), akizungumza na Mwenyekiti wa umoja wa asasi zisizo za serikali (NGO's) wilayani humo, Edward Loure (katikati), wakati wa kikao cha mwaka cha asasi hizo, katika kata ya Terrat juzi. Kulia ni Mjumbe wa umoja huo, Justin Robert. **PICHA: GIFT THADEY**

# Uganda yajifunza Tanzania sheria ya ndoa

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WABUNGE kutoka Uganda wametembelea Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT), kwa lengo la kujifunza sheria ya ndoa inavyotekelezwa pamoja na changamoto zilizopo na namna zinavyotatuliwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Wanawake Uganda, Sarah Opendi, akizungumza jana, alisema wamekuja Tanzania kujifunza namna sheria hiyo inavyotekelezwa kwa kuwa serikali ya Uganda iko kwenye mchakato wa kuandaa Muswada wa Sheria ya Ndoa.

Opendi alisema wanataka kupata uzoefu wa nchi mbalimbali wa namna zinavyotekeleza sheria hiyo ikiwamo Tanzania na Zimbabwe.

Alisema Uganda kuna ndoa za aina nyingi na muswada huo unategemewa kugusa jamii yote kama ambavyo Tanzania ilivyofanya, kwa kuzingatia ndoa za kidini, ndoa za kimila na ndoa za serikali.

Katibu Mtendaji wa LRCT, Griffin Mwakapeje, akiwa na menejimenti ya tume hiyo, alisema tume ina jukumu la kufanya mapitio, utafiti na kutathmini sheria, eneo la sheria au mfumo wa sheria husika na kutoa mapendekezo kwa lengo la kufanya maboresho na kuiboresha.

Aliwaeleza wabunge hao kuwa sheria ya ndoa Tanzania imetambua ndoa kama taasisi ambayo haina budi kulindwa kwa lengo la kuwa na taifa bora.

Pia alisema sheria hiyo inaweka masharti mbalimbali yakiwamo ya mke na mume kuishi pamoja kwa muda wa uhai wao.

Mwakapeje alisema tume pia, ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma kwa lengo la kuuwezesha umma kufahamu mabadiliko na maendeleo yanayotokea katika sekta ya sheria.

"Aina za ufungaji wa ndoa zinazotambuliwa ni nafasi ya mwenza wa ndoa kutoa ridhaa wakati wa kuuza mali za ndoa, masharti ya talaka na masharti ya dhana ya ndoa baada ya wahusika kuishi pamoja bila kuisajili ndoa hiyo," alisema.

Akielezea uzoefu wa Tanzania, Mwakapeje alisema sheria moja ya ndoa ilipatikana mwaka 1971 baada ya maridhiano ya wanajamii wote na kuzifuta sheria nyingi zilizokuwapo.

"Sheria zilizokuwapo kabla ni sheria za kimila, Kikristo, Kiislamu na za serikali ambazo zilikuwa zinasimamia masuala ya ndoa, hivyo Uganda wanaweza kujifunza kwetu ili na wao pia pamoja na mambo mengine, waweze kuwa na sheria moja ya ndoa tofauti na ilivyo sasa," alisema.

## Shirika UN lasaidia chuo wenye ulemavu

**Na Beatrice Shayo**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) limetoa Sh. milioni 92.6 kwa ajili ya kuboresha huduma za afya katika Chuo cha Ufundi Stadi kwa watu wenye ulemavu cha Yombo, Dar es Salaam.

Fedha hizo zimejenga ukumbi wa kupumzika wagonjwa wakati wanasubiri matibabu katika zahanati ya chuo pamoja na ununuzi wa vifaa tiba na marekebisho.

Akizungumza jana wakati wa makabidhiano ya ukumbi huo, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi Vijana Ajira na wenye Ulemavu, Prof. Jamal Adam, alisema anashukuru UNFPA kwa kuendelea kuunga juhudi mbalimbali za maendeleo kwa taifa.

Alisema wamenunua gari la mradi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya vijana na kutoa fedha ili kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa taarifa na takwimu za watu wenye ulemavu.

Prof. Adam alisema wanashukuru kwa kuendelea kuiwezesha ofisi yao kufanya mapitio ya sera na miongozo mbalimbali ya maendeleo ya vijana ambayo kwa kiasi kikubwa zitasaidia katika kutoa mwongozo wa utekelezaji wa afua zinazolenga kuendeleza ustawi na maendeleo ya vijana. Adam alisema serikali imeendelea kutoa kipaumbele masuala ya watu wenye ulemavu ikiwamo uwezeshwaji wa kiuchumi, afya, ajira, nyenzo za kujimudu na elimu ya mafunzo ya ufundi stadi.

"Serikali imeendelea kufufua vyuo vya ufundi stadi na marekebisho kwa watu wenye ulemavu vilivyokuwa vinafanya kazi na vile vilivyokuwa vimefungwa kwa muda mrefu kutokana na kukwepo kwa changamoto mbalimbalii," alisema Prof. Adam.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA, Mark Schreiner, alisema wamejitolea kusaidia vijana hasa wenye ulemavu kwa kuwawekea mazingira wezeshi na kupata huduma za afya kama ilivyoelekezwa katika mpango mkakati wa Umoja wa Matifa kuhusu vijana.

Alisema UNFPA kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu inaunga mkono maendeleo na marekebisho ya sera, mikakati na mifumo kwa walemavu zinazolenga kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa vijana. Mkuu wa Ushirikiano wa Kimataifa katika ubalozi wa Uswizi nchini Tanzania, Holger Tausch, alisena wamebaini baadhi ya makundi yaliyotengwa wakiwemo vijana na watu wenye ulemavu yanaachwa nyuma katika mipango ya maendeleo.

Alisema kutoka na hali hiyo mpango mkakati wa sasa wa ushirikiano wa nchi mbili na Uswizi unalenga vijana na kuinua ubora wa maisha yao.

Makamu Mkuu wa Chuo, Mariam Chellangwa, alisema chuo hicho kina wanafunzi 104 wenye ulemavu wa aina mbalimbali wakiwemo wanafunzi wasioona, viziwi, wenyue ulemavu wa viungo, wenye ualbino, wenye ulemavu wa akili na wenye ulewmavu mchanganyiko.

Chelangwa aliiomba serikali na wadau wengine kufanya maboresho katika chuo hicho ili kiwe bora zaidi katika kutoa huduma. Alisema wanahitaji msaada wa gari ambalo litawasaidia kubeba wagonjwa ama sampuli za Kifua Kikuu (TB) kwa ajili ya kufanyiwa vipimo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri wawakilishi wa Tanzania mashindano CAF

**MASHINDANO** ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho yameanza wikiendi hii kwa timu mbalimbali kushuka kwenye viwanja tofauti kuanza kusaka pointi muhimu kwa ajili ya kuwania mataji hayo makubwa kwa ngazi ya klabu hapa barani.

Michuano hiyo inayofanyika kila mwaka huandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Tanzania Bara inawakilishwa na Yanga pamoja na Simba wakati KMKM inapeperusha bendera ya Zanzibar kwenye michuano hiyo.

Azam FC, Singida Fountain Gate wao wanashiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika kutoka Tanzania Bara huku Zanzibar ikiwakilishwa na Maafande wa JKU.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na CAF, Singida Fountain Gate iliangukia kwa 'ndugu' zao wa Visiwani na jana walishuka kwenye uwanja wa Azam Complex kuanza safari ya kuwania ubingwa wa Kombe la Shirikisho wakati mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wao walikuwa na kibarua cha kuwaalika St. George kutoka Ethiopia.

AS Ali Sabieh kutoka Djibouti ambayo inatumia Uwanja wa Azam Complex itawakaribisha Yanga kesho wakati Azam FC ikiwa ugenini Ethiopia kukabiliana na wenyeji Bahir Dar Kenema. Timu hizo zote zinaanzia hatua ya awali katika michuano hiyo.

Simba ambayo mwaka jana iliishia katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, inaanzia hatua ya makundi kutokana na kukusanya pointi nyingi, pia iko katika nafasi ya saba kwa ubora barani Afrika.

Baada ya kumalizika kwa msimu uliopita, wawakilishi wetu hao walifahamu wanatakiwa kufanya maandalizi yanayofanana na ukubwa wa mashindano yanayowakabili mbele yao.

Timu zote hizo sita za Tanzania zilifanya usajili bora na wengine waliboresha mabenchi ya ufundi kwa sababu wanahitaji kufanya vyema katika michuano hiyo ambayo hufuatiliwa na idadi kubwa ya mashabiki kwa soka ndani na nje ya Afrika.

Tunaamini timu zote hizo zilifanya pia mazoezi yanayoendana na ushindani watakaokutana nao, tunafahamu kila timu inajua inaingia katika michuano hiyo kusaka heshima na rekodi ya klabu husika, lakini pia kulitangaza jina la Tanzania vizuri.

Hongera kwa timu zote za Tanzania zinazoshiriki michuano hiyo kwa kukamilisha vigezo na hatimaye kupatiwa leseni za kushiriki mashindano hayo kutoka CAF, lakini pia wakikumbushwa masharti yote ya kanuni kwa msimu mzima kwa sababu ikitokea tofauti, leseni hizo hufutwa.

Hii ni hatua muhimu sana katika kuelekea katika soka la kisasa, kama ambavyo tumeshuhudia wachezaji wa Kitayosce FC ya Tabora ambayo walishindwa kukamilisha taratibu za usajili kwa kukosa leseni na hatimaye timu yao kuingia uwanjani katika mechi ya kwanza ya ufunguzi ya Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na nyota nane pekee.


Wakati umefika kwa viongozi, wachezaji na mashabiki kila mmoja kutekeleza jukumu lake kwa ajili ya kuipa timu matokeo chanya, inapotokea kila idara inakamilisha majukumu yake, basi matokeo chanya kwa timu husika ndio jambo pekee linalotarajiwa.

Mpira wa miguu sasa huendeshwa kisomi, uongozi wa kufuata mazoea au busara umepitwa na wakati, klabu zinatakiwa kujiendesha kwa kufuata kanuni, sheria na taratibu zilizowekwa na si vinginevyo, uongozi wa mazoea ulishapitwa na wakati.

Tunapenda pia kuwakumbusha wachezaji wetu kucheza kwa nidhamu, kupambana na kujituma katika dakika zote wanazokuwa uwanjani, nyota hao wanatakiwa wakumbuke michuano hii ya CAF ni daraja muhimu kwao kujitangaza kwa timu za nje, lakini pia kujitafutia namba katika vikosi vya timu za Taifa.

Pia tunapenda kuwatakia majukumu mema waamuzi na maofisa mbalimbali wa Tanzania ambao watateuliwa na CAF kwenda kusimamia michezo ya mashindano yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba SC bado haieleweki inachotaka kwa Robertinho

Na Adam Fungamwango

**MASHABIKI** wa Simba hawaeleweki nini wanataka, kati ya ushindi au mpira mzuri.

Timu yao imecheza mechi nne mpaka sasa kutoka Tamasha la Simba Day bila kupoteza, lakini ukisikia kelele huko mitaani na mitandao ya kijamii unaweza kudhani imepoteza.

Ilianza kwa kushinda mabao 2-0 Agosti 6, mwaka huu dhidi ya Power Dynamos ya Zambia siku ya Simba Day, halafu ikaenda kwenye nusu fainali ya Ngao ya Jamii kwa kuikabili Singida Fountain Gate na matokeo yakawa sare, lakini ikatinga fainali kwa penalti 4-2.

Ilifanikiwa kutwaa Ngao ya Jamii Agosti 13, mwaka huu dhidi ya Yanga kwa penalti 3-1, baada ya dakika 90 za mchezo kumalizika kwa suluhu.

Kukazuka maneno kutoka kwa baadhi ya watu wakiwamo wachambuzi wakisema Simba imecheza mechi mbili za Ngao ya Jamii bila kufunga bao lolote.

Imeanza mechi ya Ligi Kuu kwa ushindi wa mabao 4-2, ambao ni mkubwa zaidi kwa misimu mingi katika mechi zake za ufunguzi.

Mashabiki hawaangalii tena mechi moja timu imefunga mabao manne, wanapiga kelele kwa nini imeruhusu mabao mawili. Ni mabao ambayo haikuruhusu katika michuano ya Ngao ya Jamii. Bado kuna mashabiki hawaridhiki na ushindi wote huo, kisa timu haijacheza vizuri.

Katika mpira wa miguu unaweza kucheza vizuri lakini ukapoteza, ukacheza vibaya lakini ukashinda.

Meneja Habari ya Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amekiri ni kweli bado kikosi hakijaanza kucheza soka safi kwa sababu kina maingizo ya wachezaji wengi wapya.

Ni kweli, Simba ina maingizo ya wachezaji wengi ambao wanatakiwa kuanza moja kwa moja katika kikosi cha kwanza.

Lakini haiwezekani kuwaweka wote kwa mara moja kwa sababu wametoka klabu mbalimbali hivyo wanatakiwa kuingia mmoja, wawili au watatu huku Kocha Mkuu, Roberto Oliveira, akiendelea kuiamini 'uti wa mgongo' wa kikosi chake cha msimu uliopita.

Kuna baadhi ya wachambuzi wanatabiri Robertinho hawezi kufika sikukuu ya Krismasi, na baadhi ya mashabiki wa Simba wakionekana kabisa wanakerwa naye, wanataka afukuzwe kwa sababu ameshindwa kuifanya timu hiyo kucheza soka lake 'biriani.'

Wao kucheza pasi nyingi zisizo na mpango ni muhimu kuliko ushindi, inawezekana Robertinho akawa si muumini sana wa soka la pasi nyingi za kufurahisha mashabiki, lakini takwimu zinambeba.

Mpaka sasa amecheza mechi 24 za Ligi Kuu na hawajawahi kupoteza. Kwenye Kombe la FA alipoteza moja dhidi ya Azam FC. Hajawahi kupoteza mechi yoyote dhidi ya watani zake wa jadi, Yanga.

Itashangaza kama klabu itamfukuza kocha ambaye hajafungwa mechi yoyote ya Ligi Kuu Tanzania Bara tangu atue nchini kisa tu hachezi soka zuri.

Binafsi nadhani mashabiki wa Simba wanacheza ngoma ambayo hawajui inapigwa wapi.

Wanafuata midundo ya ngoma ambayo hawajui nini. Huyu huyu Robertinho ndiye aliyeipeleka Simba hadi robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kutolewa kwa mikwaju ya penalti dhidi ya waliokuwa mabingwa watetezi wa wakati huo, Wydad ya Morocco.

Nadhani kuna kikundi cha watu ndani na nje ya klabu hiyo wako nyuma ya hili la kutaka Robertinho aondoke kwa sababu wanazozijua wenyewe.

Lakini sidhani kama viongozi wa Simba wanaweza kufanya hilo kwa sasa kipindi ambacho inahitaji ushindi zaidi kuliko kitu chochote.

Msimu uliopita Simba iliukosa ubingwa kwa sababu zinazofanana na hizi ilipoachana na Kocha, Zolan Maki na ilihaha kiasi cha kupoteza mechi kirahisi mwanzoni dhidi ya KMC na Mbeya City ikaachwa.

Hata alipokuja Robertinho tayari ilikuwa imeshapitwa kwa pointi kadhaa katika kinyang'anyiro cha ubingwa.

Waswahili wana msemo wao maarufu 'akili za kuambiwa changanya na zako.'

HABARI KITAIFA

# TEF yataka ushirikishwaji mchakato kanuni za habari

**Na Joseph Mwendapole**

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, ameshauri mchakato wa kutengeneza kanuni za habari ukamilike mapema iwezekanavyo na ameomba serikali ishirikishe wadau.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za Jukwaa hilo zilizopo jijini Dar es Salaam.

Balile alisema mwenye jukumu la kusimamia na kukamilika kwa kanuni hizo ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

"Tungependa kanuni za habari zipatikane angalau kufika Oktoba mwaka huu, kwa kuwa Waziri wa Habari halazimishwi na sheria kuhusisha wadau kwenye kutengeneza kanuni hizo, lakini akitushirikisha litakuwa jambo jema.

"Safari hii suala la kanuni za habari halipelekwi bungeni linaishia kwake, kwa hiyo wadau wa habari watafurahi kama ataamua kuwashirikisha kwenye utungaji kanuni," alisema.

Balile alisema baada ya Bunge kupitisha Marekebisho ya Sheria ya Habari, kinachofuata ni kuomba fursa ya kukutana na serikali kwa ajili ya kupendekeza mambo gani yaingie kwenye kanuni.

Alisema miongoni mwa mambo ambayo wadau wa habari wangependa kuona yanaingia kwenye kanuni mpya na kuanza kutumika ni pamoja na suala la leseni ya magazeti kuwa zaidi ya miaka mitano tofauti na ilivyo sasa.

"Tutashauri serikali kwamba, kanuni zetu zielekeze kuwa leseni pamoja na kitambulisho cha mwanahabari (press card), zidumu kwa zaidi ya miaka mitano.

"Makosa ya kitaalumu yanapaswa kubaki kwa wanataaluma wenyewe, hili litasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani," alisema.

Balile alisema eneo lingine ambalo waandishi wa habari wanatarajia liingie kwenye kanuni ni umiliki wa hisa katika vyombo vya habari kutowekewa mipaka.

Alisema siyo jambo rahisi kwa mwekezaji kutoka nje awekeze kwenye vyombo vya habari halafu asiwe na sauti, huku akitoa mfano wa uwekezaji wa bila kiwango cha asilimia katika maeneo mengine ikiwamo mitandao ya simu.

"Sheria inataka mwekezaji kutoka nje ya nchi amiliki hisa isiyozidi asilimia 49. Jambo hili linapunguza uwekezaji kwenye vyombo vya habari kwa sababu wawekezaji wataogopa kuja kuwekeza hapa nchini.

"Tutamshauri Waziri Nape kwamba, mwekezaji kwenye vyombo vya habari asiwe na ukomo kama ilivyo kwenye mitandao ya simu na maeneo mengine ili kuvutia uwekezaji zaidi kwenye sekta ya vyombo vya habari," alisema Balile.

Pia alisema, miongoni mwa mambo mazuri kwenye sheria ya sasa ni kuruhusu mwandishi wa habari kumshitaki mtoa taarifa endapo atakataa kutoa taarifa inayotakiwa na mwanahabari.

"Kuna maofisa wa serikali ambao wakitakiwa kutoa taarifa kwa wanahabari, wanagoma kufanya hivyo, lakini lazima wafahamu kwamba kwa sheria ya sasa, mwanahabari anaweza kumburuza mahakamani ofisa wa serikali ambaye hatatoa taarifa inayotakiwa," alisema Balile.



Mratibu wa vituo vya taarifa na maarifa vya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Jacqueline Mtesha (kushoto), akizungumza katika semina ya waandishi wa habari Mabibo Dar es Salaam juzi, yenye lengo la kutoa ufafanuzi wa shughuli zinazofanywa na vituo hivyo kwenye jamii. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Google, NMB kuwawezesha wananchi ununuzi simu janja

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Google, Benki ya NMB na Vodacom Tanzania PLC wameungana kuimarisha mapinduzi ya kidijitali kwa kuwezesha upatikanaji wa simu janja kwa bei nafuu nchini.

Wateja wa Vodacom watalipia kuanzia Sh. 20,000 kupatiwa simu janja zinazoweza kutumia mtandao wa 4G na hivyo kuwezesha kunufaika na fursa zinazopatikana mtandaoni.

Mkurugenzi wa Fedha wa Vodacom Tanzania, Hilda Bujiku alisema jana kuwa mpango huo mpya uliopewa jina la 'Miliki Simu, Lipa Mdogo Mdogo' ambao ni ushirikiano NMB na Android (mfumo wa uendeshaji wa Google kwa vifaa vya mkononi), unakwenda sambamba na lengo la serikali ya ujumuishi wa kidijitali.

"Maono yetu daima yamekuwa kuipeleka Tanzania kwenye ulimwengu wa kidijitali na kubadilisha maisha kupitia teknolojia, kwahiyo, ushirikiano huu unakwenda sambamba na adhma yetu ya kuwafungulia wateja wetu fursa zinazobadilisha maisha," alisema Hilda na kuongeza kuwa:

"Tunaamini ushirikiano huu utaleta mageuzi katika upatikanaji wa simu janja kwa wale ambao bado hawajanufaika na zana hizi za kidijitali.

"Tumeazimia kuwezesha wateja milioni moja kumiliki simu janja zenye uwezo wa 4G katika mwaka huu wa fedha pekee, na hivyo kuchangia kupunguza pengo kati ya wanaotumia na wasiotumia intaneti nchini," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mikopo ya simu ni mbinu inayowezesha umiliki wa simu janja kirahisi na kwa gharama nafuu kupitia malipo ya siku au ya wiki kwa kima kidogo cha hadi Sh. 900 huku mtumiaji akifurahia manufaa yanayokuja na kuunganishwa kidijitali.

Mkuu wa Android wa Ushirikiano wa Kimajukwaa Afrika Mashariki, Martin Njoroge, alisema "..lengo la Android daima limekuwa kuwawezesha watu kupitia huduma za kompyuta.

"Ufikiaji wa fursa zilizo kwenye intaneti ni muhimu sana kwa ukuaji wa kiuchumi na ujumuishaji wa kijamii katika nchi yoyote ile. Tunaamini kwamba ushirikiano huu utawaleta Watanzania wengi mtandaoni na kuwasaidia kutumia fursa zinazopatikana mtandaoni," alisema.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema "...ubia huu wenye tija ni sahihi kabisa kwa kuwa Vodacom itawapatia wateja wake mpango wa kulipia simu janja, hivyo kuwezesha kupanda daraja na kumiliki simu janja kupitia malipo ya awamu na kufungua uchumi wa kidijitali na kutengeneza fursa za ziada kwa Watanzania."

Aliongeza kuwa ubia huo unakwenda sambamba na ajenda ya benki hiyo ya ujumuishwaji wa kidijitali, maarufu Teleza Kidijitali.

Wateja watachukua simu zao katika maduka ya Vodacom baada ya kulipa kianzio cha Sh. 20,000 na kutakuwa na kwa wateja za MB 100, dakika 10 za kupiga mitandao yote na SMS 10 zitakazotumika ndani ya saa 24 pindi watakapokamilisha marejesho kwa wakati.

Iwapo mteja hatofanya marejesho kwa wakati, Vodacom itafunga kifaa hicho. Hali kadhalika, simu ikifungwa, hatoweza kuwasiliana na huduma kwa wateja na kutumia M-PESA.

# Katibu Mkuu asisitiza viwango miradi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Gabriel Migire, amewataka wakuu wa taasisi zilizo chini ya sekta hiyo kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na kuhakikisha inakamilika kwa wakati na kwa viwango.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa utiaji saini mikataba ya utendaji kwa mwaka 2023/24 baina yake na wakuu wa taasisi, Migire alisema ufuatiliaji na usimamizi utapunguza ucheleweshaji hasa kwenye kukamilika kwa kuwa changamoto zitakazobainika wakati wa utekelezaji zitapatiwa ufumbuzi mapema.

"Wataalam wako kwenye ukaguzi kila siku lakini utashangaa viongozi wakuu wakikagua miradi ndio wanabaini changamoto zilizopo. Nendeni mkawatumie wataalam hao vizuri na kuwapo na ratiba maalum zinazotambulika za ukaguzi ili mbaini changamoto mapema na kuzitafutia ufumbuzi mapema pia," alisema.

Aidha, Migire alisisitiza pia umuhimu wa nidhamu katika matumizi ya fedha. Alisema ni jukumu la wakuu wa taasisi kuhakikisha fedha zinatumika vizuri kwa kuweka vielelezo sahihi baada ya matumizi ili kupunguza hoja ambazo zimekuwa zikiibiwa kila mwaka na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG).

Mkurugenzi Msaidizi Ufuatiliaji na Tathmini Sekta ya Uchukuzi, Devota Gabriel, alisema tathmini iliyofanyika kwa mwaka 2022/23 imeonyesha taasisi zimefanya vizuri kwenye usimamizi wa miradi na mafunzo kwa watumishi hali inayoongeza morali za watumishi.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Uendelezaji Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KADCO), Christina Mwakatobe aliishukuru serikali kwa kuendelea kuweka vigezo kwa wakuu wa taasisi kwani vinawafanya kujitathmini katika utendaji kwa kila hatua ya utendaji.

Utiaji saini kwenye utendaji umefanywa kati ya Katibu Mkuu na wakuu wa zaidi ya taasisi 11 zinazosimamiwa na sekta ya uchukuzi.




Kaimu Meneja wa benki ya NMB Kanda ya Ziwa, Dickson Richard (katikati), akitoa elimu ya mikopo kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Mwanza jana, ambao pia ni wanachama wa Jukwaa la klabu ya biashara inayoendeshwa na benki hiyo. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Serikali yajipanga kuongeza uzalishaji mkonge

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya Rais Samia Suluhu Hassan kufuta mashamba pori Kilosa mkoani Morogoro, Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), imeagizwa kuongeza mashamba kwa wakulima wadogo hali itayosaidia kuongeza uzalishaji, imeelezwa.

Hatua hiyo ya Rais imeisaidia TSB kugawa mashamba kwa wakulima 983 wilayani Korogwe mkoani Tanga na wengine zaidi ya 3,000 wamegawiwa wilayani Kilosa.

Mkurugenzi Mkuu wa TSB, Saddy Kambona, alisema hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya TSB na mwelekeo wa mwaka huu wa fedha.

"Kitendo cha Mheshimiwa Rais kufuta mashamba pori wilayani Kilosa na kuiongezea mashamba TSB kwa ajili ya kuwagawia wakulima wadogo walio tayari kulima mkonge, kitaongeza uzalishaji wa zao hili,"alisema.

Kambona alitaja jitihada zingine zilizofanywa na serikali kwenye mkonge ni pamoja na kushusha riba kwenye mabenki ya biashara kwa mikopo inayoelekezwa katika kilimo na kuleta unafuu mkubwa kwa wakulima.

"Riba kwa mikopo ya kilimo sasa kwa ujumla haizidi asilimia tisa. Jitihada nyingine ni kununua mitambo mipya ya kuchakata Mkonge (Korona) na kufufua mitambo ya kuchakata mkonge ya mashamba ya Kibaranga wilayani Muheza.

"Nyingine ni shamba la serikali la TPL lililoko Kata ya Bwawani wilayani Arumeru, Arusha ambalo linasimamiwa na kuendeshwa na TSB,"alisema

Alisema mitambo hiyo itasaidia kuongeza uzalishaji wa mkonge na hivyo, kuwezesha kufikiwa kwa lengo la uzalishaji lililowekwa na serikali.

Kuhusu kuimarisha masoko ya ndani, alisema hilo ni jambo la muhimu katika kuchochea ukuaji wa uzalishaji wa mkonge nchini.

"Ni lazima tuendelee kuhamasisha wawekezaji mbalimbali kuwekeza katika viwanda vya kuongeza thamani katika mnyororo wa thamani wa zao la mkonge ili kuongeza matumizi yake na hivyo, kuchagiza kukua kwa kilimo cha mkonge.

"Lakini ni jukumu letu pia, kulinda viwanda vichache vilivyopo. Kwa sasa takriban asilimia 70 ya mkonge unauzwa nje kama malighafi kabla ya kuongezwa thamani,"alisema.

Hata hivyo, alisema kwa sasa hali ya masoko ya zao la mkonge ni nzuri ambapo mwaka huu, mauzo ya ndani ya zao hilo ni zaidi ya Sh. bilioni 23 na mauzo ya nje ya nchi ni zaidi ya Dola milioni 41, kuanzia mwezi Januari hadi mwezi Juni mwaka huu.

Mkurugenzi huyo alisema mwelekeo wa serikali ni kuhakikisha wakulima wadogo wanalima zao hilo ili kuiwezesha Tanzania kushika nafasi ya kwanza katika ulimaji wa mkonge duniani kutoka nafasi ya pili ya sasa.

# CCM Mkoa wa Iringa kuwa na ofisi kila kata

**Na Halfani Chusi**

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Iringa (NEC), Salim Abri, amesema chama hicho kimeweka mkakati maalumu wa kuwa na ofisi kila kata ili kusaidia kufanikisha utekelezaji wa shughuli za kisiasa.

Katika mkutano maalumu wa mafunzo uliowakutanisha wajumbe zaidi ya 700 wa Halmashauri Kuu zote za CCM za wilaya na mkoa huo, Abri aliweka wazi dhamira hiyo ya chama.

Alisema mkakati walionao ni kuona kila kata inapata ofisi ili kujiweka katika ramani nzuri ya kushinda hata katika chaguzi zinazokuja.

"Tukitaka kuimarisha chama chetu, lazima tuwe na maeneo na ofisi nzuri hasa ngazi ya kata, tumekaa na kamati ya siasa ili kupata tathimini katika kata zetu zote 107, ni zipi zina ofisi na zipi zimejiandaa kuanza ujenzi na zile ambazo hazina kabisa.

"Mkoa wetu una kata 107, kati ya hizo ni kata 12 ndiyo zipo vizuri zinazohitaji ukarabati ni 69 na zenye viwanja lakini hawajaanza ujenzi ni 16" alisema Abri.

Alisema wamekubaliana kuwe na ramani elekezi kwa ajili ya ofisi za kata, Mkoa wa Iringa na wamekubaliana hadi kufikia maadhimisho ya miaka 50 ya CCM kwa kiwango kikubwa wawe na ofisi hizo.

# Wanaotumikisha watoto kazi hatarishi waonywa

**Na Steven William,** MUHEZA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Dk. Juma Mhina, amewaonya watu wanaotumikisha watoto kazi ngumu au hatarishi na kuwataka kuacha mara moja.

Katika taarifa yake juzi, kiongozi huyo alisema yeyote atakaye kamatwa atatozwa faini ya Sh. milioni tano ama kifungo cha miezi sita jela.

Dk. Mhina amewaonya madalali wa machungwa na wamiliki wa mashamba ya zao hilo, wafanyabiashara wamiliki wa vyombo vya usafiri, wazazi na wananchi kuacha kuwatumikisha watoto wadogo kazi za mashambani na kupakia machungwa katika malori ya mizigo.

Alisema kufanya hivyo ni kinyume na Sheria ya Mtoto Ibara ya 13 iliyofanyiwa mapitio mwaka wa 2019 ambayo inabainisha wazi kuwa ni marufuku mtu yeyote kumwajiri mtoto ama kumfanyisha kazi yeyote ambayo ina madhara ya kiafya kwa mtoto.

Mkurugenzi huyo alisema msako mkali unaendelea kwa kushirikiana na vyombo vya dola na atakayekamatwa anamtumikisha mtoto kazi za shamba ama kazi za ndani, atashitakiwa na kutozwa faini ya Sh. milioni tano ama kifungo cha miezi sita jela ama vyote kwa pamoja faini na kufungwa jela.

Dk. Mhina aliwataka wazazi na walezi wote kukaa na watoto wao vizuri kwa kuhakikisha wanawapa elimu, malezi bora na kuwafundisha maadili mema na siyo kuwanyanyasa kwa kuwatumikisha katika ajira hatarishi.

Aliwakumbusha kuwa watoto wadogo ni hazina kwa taifa na ndiyo viongozi wa kesho wa chama na serikali, hivyo wanapaswa kulelewa katika misingi na maadili mema ikiwamo kulindwa ili wasipotoke kimaadili. Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, alisema jukumu la wazazi ni kuhakikisha wanawapa elimu na malezi bora watoto wao ili kuwaepusha na mmomonyoko wa maadili.

Mfaki aliwaagiza Maofisa Watendaji wa Kata na Vijiji kuhakikisha haki za watoto zinalindwa na kukemea vitendo vya uonevu au unyanyasaji vinavyofanywa na baadhi ya watu kama vile ubakaji na ulawiti.



# Tembo 69 wavamia kijiji, wananchi wahaha

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUNDI la tembo 69 limevamia kijiji cha Mtitaa, Bahi mkoani Dodoma na kuzua taharuki kwa wananchi huku serikali ikibainisha hatua ilizochukua ikiwamo kutoa elimu kwa wananchi na kutambua shoroba.

Tukio hilo lilitokea juzi kijijini hapo majira ya saa 4:00 asubuhi na kuzua taharuki kijijini hapo.

Akizungumza na Nipashe kuhusu tukio hilo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Godwin Gondwe, alisema hakuna madhara yaliyojitokeza kwa binadamu licha ya wananchi kuwafukuza kama ngombe kabla ya askari wanyamapori kufika kunusuru hali hiyo.

Alisema katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imetuma timu ya askari 24 ambao wamepiga kambi kwenye eneo hilo ili kutoa elimu ya kina kwa wananchi namna ya kukabiliana nao ili wasilete madhara.

"Tunashukuru hakuna madhara kwa binadamu yaliyojitokeza na nimetoka kufanya kikao na wananchi leo (jana) kwamba wakiona tembo wasipige kelele maana wanaweza kusababisha madhara kwao, tunashukuru wale tembo walikuwa na watoto pamoja na kelele zile za wananchi lakini hawakusababisha madhara.

"Tukio jingine lililonishangaza ni wananchi kutumia fursa ya tembo kushambulia shamba la zabibu na wao wakavamia na kuanza kula zabibu za Albert. tumewaasa wananchi kujiepusha na tabia hii," alisema. Alisema kwa sasa maofisa hao wa TAWA wamefanikiwa kuwadhibiti na kuelekea hifadhi ya Ruaha.

"Kwa mwaka huu Mtitaa ni mara ya kwanza kupita tembo lakini Chifutuka tayari wamepita mara mbili, tumekuja na mkakati wa kutambua ushoroba ili wananchi wasijenge wala kufanya shughuli zozote kwenye njia hizo za tembo," alisema. Alibainisha pia watapewa elimu ya namna ya kukabiliana nao kwa njia za asili kwa kuchoma pilipili iliyochanganywa na kinyesi cha ng'ombe kwenye mashamba yao.

"Tutaanza kutoa elimu kwa wananchi wa vijiji hivi hasa vinavyosumbuliwa na tembo na mkakati ni kutoa elimu kwa wilaya nzima ili kwenye zile shoroba za tembo kuwe na tahadhari, nimshukuru Rais kwa kuunda taasisi hii ya TAWA na Waziri wa Maliasili kwa kuleta timu ya ziada kutuliza hali na kutoa elimu ya namna bora ya kukabiliana nao,"alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mtitaa, David Makua, alisema tembo hao walizua taharuki na kuvamia shamba la mihogo lenye ukubwa wa ekari moja na zabibu ekari tatu za kiwanda cha mvinyo cha Mkwambi.



Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel (aliyenyoosha mikono), akitoa ufafanuzi kwa Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu Uganda, Dk. Flavian Zeija (kushoto), alipofanya ziara katika Makao Makuu ya Mahakama hiyo, jijini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Waziri azionya idara za fedha halmashauri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amezinyooshea kidole idara za fedha kwenye halmashauri na kuzitaka kuchunguza mawakala wa kukusanya mapato ili kuondokana na upotevu wa mapato.

Kairuki alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha watunza hazina na wahasibu wa sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuhusu ukaguzi wa hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha Juni, 2023.

"Tumekuwa tukisikia kuna changamoto nyingi huko haswa kwa Maofisa waidhiniwa na mawakala ambao tumewapa mamlaka ya kukusanya mapato kwa niaba ya halmashauri zetu kuna wengine wanazo hadi mashine mbili mbili, inawezekana wengine tunawajua, ni vyema tukafuatilia mienendo ya maofisa wetu," alisema.

Alibainisha kuwa ni muhimu utaratibu unaotumika kuwapata mawakala wa kukusanya mapato kuangalia vyema vigezo vinavyotumika ikiwamo historia zao za masuala ya kifedha.

"Tuangalie historia zao katika masuala ya kifedha, unaweza kukuta ni wezi tu, au wana historia ambayo si safi sana, lakini hatujachunguza halafu tumekuja kumpa madaraka ya kufanya kazi kubwa kwa niaba ya halmashauri," alisisitiza Kairuki. Aliagiza kufuatiliwa kwa mashine za POS ambazo zimefungwa hazifanyi kazi ili kujua zipo wapi na kama ni kweli hazitumiki.

"Kuweni macho na wale mawakala wanaokusanya fedha bila kuzipeleka benki, unakuta mwingine muda mrefu yupo katika mfumo, wapo wengine ambao pengine nimekuwa nikiingia naona mtu amekaa siku mbili au tatu, hajapeleka makusanyo yake benki hivyo ni lazima mfuatilie kwa karibu zaidi," alisema.

"Najua mmeona baadhi ya maeneo wamekwenda mahakamani wamefunguliwa kesi kwa mfano Ilala, Dar es salaam watu 17 walienda kati ya hao wote ni watu wa idara ya fedha," aliongeza.

Kuhusu hoja za ukaguzi, Kairuki aliwataka kutimiza wajibu wao ipasavyo na kuhakikisha wanafunga hesabu inavyotakiwa na isitokee hoja yoyote.

Naye Mwenyekiti wa Wahasibu, George Mashauri, alisema wamefanya mapitio ya ufungaji wa hesabu kwa halmashauri

# Kikwazo mapambano ya Ukimwi chatajwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MOJA ya sababu ambazo zinachangia Tanzania isifikie malengo yake katika kupunguza maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) ni kutowajumuisha wazee kwenye miradi mbalimbali ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo, imeelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika linalojihusisha na masuala ya wazee la HelpAge Tanzania, Smart Daniel, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungua kikao cha wadau kujadili vikwazo vinavyowakabili wazee wanaoishi na VVU nchini.

Alisema hivi sasa licha ya uwepo wa wazee wanaoishi na virusi vya ukimwi nchini bado lipo tatizo la kundi hilo kutojumuishwa katika miradi mbalimbali ya mapambano dhidi ya maambuzi ya VVU.

"Kama kundi hili halijapewa kipaumbele kwenye mapambano dhidi ya VVU, tunawezaje kufikia malengo ya kuongeza idadi ya wanaotumia dawa za kufubaza virusi vya ukimwi na kuzifikia huduma zote za masuala ya ukimwi kwa asilimia 95 ifikapo 2030.

"HelpAge kwa kushirikiana na TACAIDS tumeandaa mkutano huu kwa kuwakutanisha wadau wanaojihusisha na masuala ya ukimwi ili kuangalia ni kwa namna gani wazee wanashindwa kuzifikia huduma bora za ukimwiI nchini ili kuzipatia ufumbuzi," alisema.

Alisema miradi ambayo inatekelezwa hivi sasa mingi imejikita katika kuhudumia makundi mengine ya vijana wa rika balehe na wazee hawapewi kipaumbele.

Pia alisema katika kikao hicho wameshirikisha pia wizara ya Afya, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Baraza la watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi nchini (NACOPHA) ili kujadiliana kwa pamoja na kuja mkakati maalum wa kusaidia wazee kupata huduma bora.

Alisema mkakati huo utasaidia kupunguza kero mbalimbali kwa wazee wanaoishi na virusi vya ukimwi ikiwemo unyanyapaa na umaskini.

Naye Mkurugenzi Mwandamizi wa Ushirikishwaji wa Jamii na Sekta Binafsi Baraza la Watu Wanaoishi la Virusi vya Ukimwi (NACOPHA), Mathew Kawogo, alisema mkakati wa kitaifa unahitajika ili wazee wenye Ukimwi kupata nauli za kufika kwenye vituo vya utoaji huduma.





## ZMBF, Afya Checkers kunogesha matembezi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF) imeingia makubaliano ya ushirikiano na Afya Checkers ya Dar es salam kwa ajili ya kutoa huduma za afya kupitia kampeni ya 'Afya Bora, Maisha Bora' inayoendeshwa na taasisi hiyo kupitia matembezi ya 'Mariam Mwinyi Walkathon'.

Matembezi hayo ambayo ni mwendelezo wa kampeni ya Mke wa Rais, Mama Mariam Mwinyi, aliyokua akiifanya kupitia matembezi ya kila mwisho wa mwezi, yanatarajiwa kufanyika Septemba 30, mwaka huu, kwa kutanguliwa na kambi ya matibabu itakayofanyika Septemba 28 na 29.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini wa makubaliano hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa ZMBF, Fatma Fungo, alisema hatua hiyo inalenga kuyaimarisha matembezi hayo na kutoa fursa kwa wananchi kupata huduma za afya.

Aidha, Fungo alisema katika awamu ya kwanza ya kampeni hiyo, matembezi hayo yalifanyika katika wilaya zote za Zanzibar kwa kushirikisha wadau kwa lengo la kuimarisha afya zao.

"Mara ya mwisho matembezi hayo yalifanyika kisiwani Pemba ambapo watu zaidi ya 3,000 walijitokeza kumuunga mkono Mama Mariam Mwinyi katika matembezi na mazoezi ya viungo ili kujenga miili yao," alieleza Fungo.

Akizungumzia marathoni hiyo, alisema itafanyika kila baada ya miezi mitatu na kwa lengo la kuyaimarisha, yatajumuisha utoaji wa huduma za uchunguzi, upimaji na matibabu ya maradhi mbalimbali zitakazotolewa na wataalamu wa afya kutoka ndani na nje ya Zanzibar. "Ili kufikia madhumuni ya kampeni hii, tumeamua kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Afya Checkers ili kuendelea kujenga misingi ya kuimarisha afya za wananchi wenzetu ikiwa ni miongoni mwa malengo ya taasisi yetu", alisema Fungo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Afya Checkers, Dk. Isaac Maro, alisema watatumia uzoefu walionao kufanikisha kampeni hiyo ili kutoa fursa kwa wananchi kupata huduma za afya na matibabu kwa urahisi.

Alitaja baadhi ya huduma zinazotolewa na taasisi hiyo ni pamoja na uchunguzi wa maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza ikiwamo ya UVIKO - 19 na huduma za utengamano kwa watoto wenye ulemavu kupitia shule.

# Huduma za DAWASA zamkuna Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa kushiriki kwenye kongamano la utekelezaji wa programu ya uwekezaji kwenye sekta ya maji Zanzibar.

Programu hiyo ilizinduliwa mwaka 2022 kwa kuweka banda la kuonyesha utekelezaji wa mipango mbalimbali ya mamlaka na mafanikio ya sekta ya maji katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na baadhi ya maeneo ya Tanga na Morogoro.

Kongamano hilo limeandaliwa na Wizara ya Maji, Nishati na Madini ya Zanzibar kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya maji. Mgeni rasmi alikuwa Dk. Mwinyi.

Lengo la kongamano hilo ni kukutanisha wadau wa maji kujadili na kubadilishana uzoefu katika masuala mbalimbali pamoja na kutambua maeneo ya ushirikiano na kaulimbiu ya kongamano ni 'Kuongeza Kasi ya Mabadiliko Katika Kufikia Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Maji Chini ya Ardhi Pamoja na Uhimilivu kwa Wote.

Akizungumza kwenye kongamano hilo, Rais Mwinyi alipongeza DAWASA kwa kushiriki kongamano hilo na kuitaka Wizara ya Maji Zanzibar kuimarisha huduma ya usambazaji wa maji na usafi wa mazingira kupitia ubunifu na teknolojia ya kisasa na miundombinu pamoja na uimarishaji wa tasisi za usimamizi wa maji. "Kama mnavyoelewa tafiti nyingi zimefanyika katika maeneo ya Unguja na Pemba na kubaini vyanzo vya maji chini ya ardhi vinavyoridhisha, hivyo naagiza wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar kuendelea kufanya kazi kwa karibu na wataalam mbalimbali wa sekta ya maji na kuandaa mpango maalum wa maji yaani "Water Master Olan, alisema Dk. Mwinyi.

DAWASA katika kongamano hilo imepata fursa ya kutoa elimu ya huduma ya maji pamoja na kuelezea mafanikio ya sekta ya maji katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na baadhi ya maeneo ya Morogoro na Tanga kupitia kutekeleza miradi ya kimkakati.

Akizungumza wakati Rais Mwinyi alipotembelea banda la DAWASA, Meneja Usambazaji Maji wa DAWASA, Mhandisi Tyson Mkindi, alisema mamlaka imejipanga kufikia asilimia 95 ya upatikanaji wa huduma ya maji katika eneo lake la kihuduma.

Alisema mamlaka inajitahidi kupunguza kiwango cha upotevu wa maji kupitia uboreshaji wa huduma wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). "Serikali imeelekeza kufikia mwaka 2025 tufikie asilimia 95 na mamlaka imejipanga kutekeleza miradi ya kimkakati hasa maeneo ya pembezoni yaliyokuwa bado ili kufikia malengo hayo," alisema Mkindi.



Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Kinondoni, wakikagua mradi wa maji Mkaongo-Bagamoyo unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) juzi. Wa (tatu kushoto) ni Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima mwani kupewa elimu kuongeza tija katika uzalishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imedhamiria kuwapa elimu wakulima wa mwani ili kulima kisasa na kupata tija ya zao hilo na kuongeza mnyororo wa thamani.

Mwenyekiyi wa Jumuiya ya Wakulima wa Mwani wa kikundi cha Tusikimbiane Bungi, Wilaya ya Kati Unguja, alisema katika kufikia malengo ya serikali ya uzalishaji wa mwani ni lazima wakulima kulima kisasa zaidi.

Alisema wameamua kuwapa elimu wakulima hao ili kufahamu namna gani bora ya kulima kilimo kibiashara na kuacha kulima kwa mazoea.

Wakulima wa mwani wengi Zanzibar, alisema wanalima kilimo hicho lakini walikuwa hawajui ukulima wenye tija hasa kufunga unapokuwapo katika maji ya bahari.

Alisema wakulima wengi wa zao hilo wanalima kwa kutumia mbegu iliyokuwapo lakini serikali iko katika hatua za kufanya utafiti kuona wakulima wananufaika zaidi.

Wakulima wa kikundi hicho walisema watayafanyia kazi mafunzo hayo kunufaika na kilimo hicho kwani kinamama walowengi wa kijiji hicho hutumia zao la mwani kama kilimo cha kuwapatia fedha .

Mwatima Pandu alisema bado wanakabiliwa na ukosefu wa vifaa vya ukulima huo na mbegu bora zakisasa.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Rasilimali za Baharini, Dk. Zakaria Ali Khamis, alisema katika kuchukua hatua za kuboresha zao hilo, tayari ukaguzi wa eneo ambalo linatarajiwa kufanyiwa maboresho ya miundombinu ya maabara kwa ajili ya utafiti ili kuwa na tija .

Pia alisema kwa sasa serikali iko katika mipango ya kuanzishwa kwa kituo cha utafiti cha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ya zao hilo ili kuwa na mabadiliko katika kulifanya kuwa bora .

Dk, Khamis alisema katika kufanikisha uzalishaji wa zao kutawezesha kuondoa changamoto za wakulima ikiwamo ongezeko la joto la maji ya bahari linalosababisha kupungua kwa uzalishaji.

"Kupitia mradi wa AFDA, Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi imeamua kuanzisha maabara ya kisasa ili kupandikiza mbegu za zao hilo katika maabara na kutoa mbegu ambazo zitastahamili na kuhimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuongeza thamani na uzalishaji wa mwani," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



BURNA BOY AWASHANGAA Uk.14

JUMAMOSI AGOSTI 19, 2023



# HAKUNA MWINGINE

DIAMOND Platnumz ni jina linalotikisa tasnia ya muziki ukanda wa Afrika mashariki na kati. Ubunifu na umahiri wake wa kuimba na kucheza ni sehemu zinazowafanya mashabiki wake kupagawa.

Kutokana na vionjo vyake vitamu katika nyimbo zake, jina lake limezidi kupaa na kupata umaarufu duniani kote na kumfanya kuwa miongoni mwa wasanii wachache wanaopata mialiko mingi ya kimataifa.

Hivi karibuni imeelezwa atakwenda nchini Marekani kushiriki katika tamasha kubwa la muziki wa kiafrika linaloitwa Afro Nation ambalo linawakutanisha wasanii wakubwa duniani.

Diamond alikuwa kimya katika kipindi fulani, lakini alirudi upya na kutoa singo mfululizo ambazo zinatamba katika majukwaa ya muziki.

Kualikwa kwenda kutumbuiza katika tamasha hilo, ni dalili nzuri kwamba yeye ni simba halisi anayeweza kutamba bila hofu.

Hata mwenyewe aliahidi kwamba kurudi kwake ni ishara kwamba anataka kuwa namba moja kila wakati na nyimbo zake zitaongoza katika chati za muziki.

Hata hivyo, benchi lake linalomuongoza linapaswa kupewa pongezi kutokana na kazi kubwa ya kumtangaza vyema na kupata kazi nzito tofauti na wasanii wengine.

BASI SAWA



## Willy Paul anafanya kusudi

MWANAMUZIKI kutoka Kenya Wilson Radido, maarufu kama Willy Paul amesema anafanya kusudi kutotoa singo mpya.

Katika taarifa yake, mwimbaji huyo amesema anataka kuonyesha jinsi gani muziki wa nchi hiyo ulivyokuwa duni bila yeye.

Amesema wakati yuko kwenye mapumziko, wanamuziki wenzake wengi wamejaribu kutoa nyimbo, lakini hawakufanikiwa kuliteka soko.

## Anna Rumba azidi kukomaa



MWIMBAJI anayekuja kwa kasi kwenye muziki wa Injili, Anna Rumba, amesema albamu yake ya 'Mbingu Zimekukubalia' inazidi kumpatia miujiza.

Akizungumza na BT jana, Rumba amesema mafanikio aliyoyapata tangu kuachia albamu hiyo, amepata uwezo wa kuandaa video ya kwanza.

"Huduma yangu inazidi kuchanua na mpaka sasa albamu inafanya vizuri, nimetoa video ya kwanza ya wimbo wa Mbingu Zimekukubalia wimbo ambao umebeba jina la albamu," amesema Rumba.



## Harmonize afurahia Single Again

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Harmonize, amesema ngoma yake 'Single Again' umemfanya kujulikana duniani baada ya kushika namba moja katika mtandao wa Spotify.

Single Again ndio wimbo wa kwanza Tanzania kufikisha wafuasi milioni 5 mwaka huu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram Harmonize, amesema remix ya wimbo huo ndio inakuwa kolabo yake yake ya kwanza kwa wanamuziki wa nje mwaka huu.



## Mbosso mume wa mtu

MWANAMUZIKI mwenye nguvu katika muziki wa Bongo Fleva, Staa wa Bongo Fleva, Mbosso, amesema yeye ni mume wa mtu kwani amefunga ndoa ya siri.

Hata hivyo, amekana kuwa na tabia ya kuwakataa watoto licha ya kuonekana amefanana nao.

"Mimi sina hizo tabia sasa hivi. Nina mke wangu mzuri, nimemwoa kisirisiri, nakula vizuri, nalala kwa wakati," amesema.

Ameongeza "Watoto wangu najivunia sana, nafurahia kuwa baba na mimi nawapenda sana watoto wangu. Kwanza wengine naishi nao nyumbani kwangu."

## Ajali ilivyowateketeza mastaa Bongo

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA ni moja kati ya nchi zilizojaaliwa kupata wasanii na wanamuziki wakubwa, mahiri na tishio kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Si kwenye muziki wa dansi, taarabu, bongo fleva, na hata waigizaji, Tanzania imebahatika kupata wanamuziki ambao wameipatia heshima kubwa nchi hii kwenye masuala ya muziki.

Hata hivyo kwa bahati mbaya wengi wao wamefariki kwa sababu mbalimbali, ikiwemo maradhi na ajali.

Leo tutawaangalia wanamuziki na wasanii bora kabisa nchini, ambao walifariki dunia kutokana na ajali za barabarani.

**Salum Abdallah**

Ni mmoja wa waasisi wa muziki wa Tanzania. Salum Abdallah alizaliwa tarehe 19 mwaka 1928 mjini Morogoro kwa baba Mwarabu raia wa Yemen na mama mwenyeji wa mkoa wa Morogoro.

Hadi leo hii, licha ya kwamba alifariki mwaka 1965, lakini baadhi ya nyimbo zake ni maarufu hadi leo. Nyimbo hizi ni 'Mkono wa Idd', 'Shemeji Shemeji huku Mwazima Taa, ' Wanawake Tanzania', 'Ngoma Iko Huku', 'Nina Mpenzi wangu Kibambaye' na nyingine nyingi.

Alifariki mwaka 1965 kwa ajali ya gari, baada ya lori lake la mchanga alilokuwa akiendesha kugonga ukingo wa daraja na kumtupa nje. Ajali hiyo ilitokea mkoani Morogoro wakati alipotoka kulikwamua lori hilo lililokuwa limekwama na kulirudisha nyumbani.

**Mbaraka Mwinshehe**

Huyu pia ni mwanamuziki aliyetokea Morogoro kama Salum Abdallah. Ni mwanafunzi wa Salum pia. Alizaliwa Moro mwaka 1944 na kutokea kuwa mwanamuziki mkubwa mno Afrika Mashariki na Kati.

Hata nchini Zaire wakati huo kwa sasa Congo DR, walimfahamu mwanamuziki huyu. Alikuwa mwimbaji na mpiga gitaa kwenye bendi ya Moro Jazz, na ilipofika mwaka 1973, aliunda kundi lake la Super Volcano. Moja ya wimbo wake bora ambao hadi leo unapendwa na vizazi vya sasa no 'Shida'.

Alifariki Januari 12, 1979 Mombasa nchini Kenya alipokuwa amekwenda kwenye kazi zake za muziki.

Gari dogo la rafiki yake alilokuwa amepanda liligonga lori lililokuwa limeegeshwa na kufariki dunia.

**Abuu Semhando**

Ni mwanamuziki mkongwe, mpiga drums wa bendi za Tanga International, Super Matimila, Tomatoma, Vijana Jazz na mwishowe African Stars 'Twanga Pepeta'.

Alifariki dunia usiku wa kuamkia Desemba 18, 2010, baada ya pikipiki aliyokuwa akiendesha kutoka kwenye onyesho la Twanga Pepeta, kugongwa na gari eneo la Mbezi Beach, Dar es Salaam na kusababisha kifo chake.

**Issa Kijoti**

Mwimbaji wa muziki wa taarabu aliyekuwa akichipukia, baada kutoa wimbo wake wa 'Usinijadili' ambao ulikuwa na kionjo kilichoondokea kuwa maarufu kilichoimbwa hata na watoto mitaani 'nichumu, nichumu tena, mwaaa', Issa Kijoti, alifariki dunia 2011, baada ya basi dogo walilokuwa wakisafiria kutoka Mbeya walikokwenda kimuziki, kugonga lori lililokuwa na mbao, ambalo basi hilo lilitaka kulipita mkoani Morogoro.

Kijoti, aliyekuwa kiongozi wa Five Star na maarufu wakati huo, alifariki dunia na baadahi ya wanamuziki wenzake.

**Sharo Milionea**

Ndiye alikuwa ameshaanza kuwa maarufu na kuanza kupata mafanikio ya kazi yake ya uigizaji wa ucheshi.

Sharo Milionea, jina halisi Hussein Ramadhani, wakati ananza kuonja mafanikio, baada ya msoto wa kufika hapo, alipata ajali mwaka 2012 katikati ya maeneo ya Segera na Muheza. Akiwa anakwenda kwao mkoani Tanga, gari alilokuwa akiendesha aina ya 'Toyota Harrier' alipokuwa akitoka kwenda Muheza, lilipinduka baada ya kuacha njia kwenye eneo linaloitwa 'Maguzonizonga', na kusababisha kifo chake.



Sharo Milionea



## Masikini: Kisebusebu, kiroho papo

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE Maisha ya kawaida, mtu unaweza kuona kama hataki kitu fulani, lakini akitokea mwingine akakihitaji, basi utaona yule asiyekitaka anabadili mawazo.

Kwenye maisha ya ndoa, kuna wanaume au wake ambao wanawanyanyasa wenzao na kuonekana kama vile wanajipendekeza sana kwao, lakini inapotokea akasikia kuna mtu pembeni anamnyemelea, anageuka mbogo.

Hii ndiyo iliyosababisha waswahili kuwa na msemo wa 'kisebusebu na kiroho papo.'

Leo tunaiangalia filamu moja kabambe iitwayo 'Masikini wa Macho.'

Denis ambaye ana mke wake wa ndoa. Anaitwa Rose. Baada ya kuoana miaka michache ikapita bila dalili zozote za kupata mimba, achilia mbali kupata mtoto.

Hili lilimfanya Denis ajione mnyonge. Akaanza kumnyanyasa mkewe. Ikafikia wakati akawa anamtukana na mwisho wake akamtimua nyumbani kwake.

Japo baada ya siku kadhaa mke alirejea na kuomba sana warudiane, lakini Denis alikataa katakata.

Rose alisalimu amri akarudi kwao. Na huko wazazi wake walikuwa wamefariki, badala yake wanaishi dada na kaka yake tu.

Baada ya muda akampata kijana mmoja ambaye ni mlemavu wa macho. Hakujali hilo. Alichojali ni upendo wa dhati.

Kijana akamsimulia maswahibu yaliyomkuta nyuma kuwa alikuwa na wazazi wake, lakini walifariki akiwa mdogo, akalelewa na kaka yake, lakini baadaye alimfukuza.

Habari hiyo ilizidi kumfanya Rose amuonee huruma kijana huyo mtanashati.

Mapenzi yao yalinoga, kiasi cha kuwashangaza wengi na kuwa kivutio pia. Kijana huyo aliitwa Lameck. Habari ikamfikia Denis, na kuna siku akawafuma laivu kabisa.

Akili ikamkaa sasa Denis na kumuomba mkewe warudiane. Mke alikataa katakata. Akamwambia sababu ambazo zilimfanya amtimue bado zipo. Denis akaunda kikundi cha maharamia kwa ajili ya kumteka Lameck na Rose pia.




# Wengi wamlilia Magoo

MKONGWE wa muziki wa Hip hop wa Marekani, Magoo anazidi kuliliwa na wengi kutokana na kifo chake cha ghafla.

Mwanamuziki huyo ambaye jina lake halisi ni Melvin Barcliff, atakumbukwa kwa ushirikiano wake na wasanii wenzake kama Timbaland, Missy Elliott na Aaliyah katika nyimbo mbalimbali.

Chanzo cha kifo chake hakijawekwa wazi, lakini baadhi ya wasanii wakubwa wameonyesha majonzi yao baada ya kusikia taarifa ya kifo chake.



## Burna Boy awashangaa

MWIMBAJI nyota kutoka Nigeria, Damini Ogulu, maarufu kwa jina la Burna Boy, amesema watu wengi nchini mwake hawaamini kama yuko kwenye kiwango cha juu sawa na wanamuziki wa muziki wa Marekani.

Burna Boy amesema albamu yake inayokuja, ni jibu lake kwa watu ambao wanamdharau.

Mwanamuziki huyo amesikitika jinsi Wanigeria mara nyingi wanavyodhani marapa wa Kimarekani pekee wanakuja juu na si yeye.

## Ronke kawa kimodo

MWIGIZAJI Mkongwe wa Nollywood, Ibironke Ojo-Anthony, maarufu kwa jina la Ronke Oshodi Oke amefunguka kuhusu safari yake ya kupunguza uzito.

Msanii huyo mahiri ametoa siri ya kufanikiwa kupunguza uzito wake kutoka kilo 110 hadi 87, wakati akihojiwa na mtangazaji maarufu, Chude Jideonwo.

"Ni daktari wangu aliyesema nipunguze uzito.Nilikuwa kama 'eleyi po ke', nilikuwa nikifanya mambo yangu tu lakini nikaanza kuwa na magonjwa ya moyo na hapo nikasema wacha nianze kufanya jambo hili."Amesema.

Ronke, chini ya uangalizi wa daktari wake, alianza safari yake ya kupunguza uzito kwa kutumia dawa maalum hadi alipofikia kilo 82, na kuhisi amekuwa mwembamba sana.





## Drake kawa mzazi bora

MKALI wa Hip hop wa Marekani, Drake ameonyesha ujasiri wa aina yake baada ya kuwaomba mashabiki kuacha tabia ya kumtupia sidiria jukwaani kwani inaweza kuleta taswira mbaya kwa mtoto wake.

Drake alikuwa na onyesho la aina yake mjini Los Angeles, aliambatana na mtoto wake Adonis ambaye alikuwa akifuatilia tamasha hilo akiwa ndani ya jingo.

"Haya sikiliza. Siwezi kuongelea sidiria usiku wa leo hapa Los Angeles kwa sababu mwanangu yuko kwenye show kwa mara ya kwanza kabisa, hivyo tafadhali weka sidiria yako usiwe unazitupa hapa." aliandika kwenye insta story yake.

## Chance The Rapper kusimulia mapito

MWANAMUZIKI wa kufokafoka Chance the Rapper, ameandaa tamasha zito ambalo litabeba ujumbe wa mabaya na mazuri aliyopitia katika maisha yake ya kimuziki.

Tamasha hilo ambalo litafanyika katika kitongoji alichozaliwa cha Apple Michigan Avenue huko Chicago, ni maalum kwa ajili ya kuadhimisha miaka 50 ya muziki wa hip hop.

Mshindi huyo wa Grammy anatarajia kuzungumzia athari za hip-hop katika maisha yake, ikiwa ni pamoja na biashara yake kama msanii wa kujitegemea.



## Ajali za watoto zaumiza trafiki

**Na Oscar Assenga,** TANGA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Tanga, limesema mkoa huo unakabiliwa na matukio ya ajali hasa kwa watoto na wanafunzi wanapotoka kwenda shuleni na wanaporejea nyumbani.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tanga, Wiliam Mwamasika, wakati akizungumzia mpango kazi wa usalama barabara kwa jiji la Tanga unaotekelezwa na Shirika la Amend Tanzania ambao umefikia asilimia 90.

Kabla ya kuzungumzia mpango huo, alishuhudia uendeshaji wa kesi katika Mahakama ya Watoto (Mahakama Kifani) kwa madereva waliovunja sheria za usalama barabarani kwa kutosimama maeneo yenye alama za watembea kwa miguu yanayotumiwa kuvuka wanafunzi.

Alisema mpango huo umekwenda sambamba na kufadhili mafunzo kwa waendesha bodaboda 300 katika Jiji la Tanga ili kuwawezesha kuzitambua sheria za usalama barabarani na namna ya kuweza kuziepuka.

Mara nyingi, alisema ajali hizo zimekuwa zikisababishwa na waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda kutokana na baadhi yao kushindwa kufuata sheria za usalama barabarani.

Alisema kutokana na tatizo hilo, jeshi hilo limejipanga kuimarisha usalama hasa kwenye vivuko wavyovukia wanafunzi nyakati za asubuhi ikiwa ni mkakati wa kutokomeza ajali ambazo zimekuwa zikipoteza ndoto zao.

"Kwa kweli sisi kama Mkoa wa Tanga, tumejipanga vizuri kuhakikisha tunatokemeza ajali za barabarani hususani kwa watoto na wanafunzi kwa kuhakikisha kila siku hasa nyakati za asubuhi kuna kuwa na askari wa usalama kwenye vivuto vya watembea kwa miguu kwa lengo kuondosha ajali hizo," alisema.

Alisema watumiaji wa vyombo vya moto wamekuwa wakipuuzia sheria za usalama barabarani licha ya kuzifahamu hivyo ni jukumu la kila mwananchi sasa wahakikishe wanazingatie na kufuata sheria za usalama ili kuweza kupunguza ajali

Meneja wa Amend Tanzania, Simon Kalolo, alisema shirika hilo limetekeleza mpango kazi wa usalama barabarani kwa Halmashauri ya Jiji la Tanga, kwa asilimia



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu (kulia), akikabidhi hati ya uteuzi kwa Mwanaharakati wa haki za binadamu na Mkazi wa Kijiji cha Mlangoni, Kata ya Garagua, Dorcas Meena baada ya kumwapisha kuwa Mjumbe wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Siha, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Walalamika wake zao kuwanyima unyumba

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BAADHI ya wanaume wanaoishi na kuendesha shughuli za kujipatia kipato katika vijiji vitano vya Kata ya Mwika Kusini, Moshi mkoani Kilimanjaro, wamelalamikia ukatili unaoendelea kufanywa na wenza wao kuwanyima unyumba kwa sababu hawana pesa za kuwahudumia.

Aidha, wameeleza masikitiko yao ya namna wanavyotekeleza kile walichokiita ukatili dhidi yao, baada ya wake zao kuweka vipandikizi vya uzazi wa mpango ili kuwazuia wasizae nao.

Wakizungumzia hali hiyo jana, wakati wa mdahalo wa jamii uliolenga kujadili nguvu na uwezo wa wanaume kusaidia kumaliza matatizo ya ukatili wa kijinsia katika Wilaya ya Moshi kwa kushirikiana na wanawake wanaharakati, wanaume hao kwa nyakati tofauti walieleza kusikitishwa na ukatili huo wa kisaikolojia ambao unaendelea kuota mizizi kila uchao.

Mmoja wa wakazi wa kata hiyo, Bariki Kimaro, alisema: "Unazungumza nini! Sasa hivi watoto wako huku (anaonyesha kwa kupiga kwa mkono bega lake), nani ana muda wa kuzaa? Wanawake wanasema hawana muda wa kuzaa, wana muda wa kutafuta pesa.

"Nazungumza ukweli na nyie kinamama mjue na Mungu anasikia. Wanafunga watoto huku (begani), hata ufanyeje hakuna mimba. Nyie kinamama mwangalie mpange muda wa kuzaa kuongeza taifa.

Baada ya kauli hiyo, Grace Kihwelo, alimjibu mzee Kimaro akisema: "Hatutaki kuzaa kwa sababu tunalea peke yetu. Nina mume ninabeba mimba peke yangu miezi tisa, naenda leba najifungua pale.

Wa kuja kuniangalia pale hakuna. Natoka hospitalini narudi nyumbani natakiwa nile uzazi miezi mitatu wa kuniangalia kwenye ule uzazi hakuna.

"Mtoto anakua anatakiwa malazi, anatakiwa elimu, haki zote za mtoto anatakiwa na anayezifanye zote ni mimi mwanamke.

Nimeshazaa mtoto wa kwanza nimekiona, nimezaa wa pili nimekiona, hivi kweli nitathubutu kuongeza wa tatu na wa nne? Kwa hiyo ziko sababu zinazotufanya wanawake na mabinti tunaokua tutumie uzazi wa mpango."

Wanaume hao wamefichua siri hiyo wakieleza kuwa hivi sasa katika vijiji hivyo, wanawake kwao ni mwendo wa matumizi ya sindano, vidonge, kitanzi na kutoshiriki ngono na waume zao.

"Pombe kali na za bei rahisi hasa hizo zinazoitwa mawingu, zimekuwa nyingi sana kwenye kata yetu, wababa na vijana wengi wanaharibika.

Hawafanyi kazi kutwa ni kulewa hakuna hatua inayochukuliwa.

Serikali inakusanya tu mapato bila kujali hali ya wananchi wao," alisema Lazaro Ngomuo, mkazi wa kijiji cha Kondeni.

Kabla ya mdahalo huo, Mratibu wa mradi wa jitihada za jamii katika kuzuia na kutoa taarifa dhidi ya watoto na wanawake, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT-Trust), Veronica Ulomi, alisema kata ambazo zimelengwa kunufaika na mradi huo ni Mwika Kaskazini, Mwika Kusini, Oldmoshi Magharibi, Kibosho Magharibi na Kirua Vunjo Kusini.

Kwa mujibu wa Ulomi, mradi huo unalenga kuchangia uboreshaji wa msaada wa kisaikolojia, haki ya kielimu na kumaliza matatizo ya kiakili yanayohusiana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto mkoani Kilimanjaro.

Aidha, mradi huo unalenga kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto kwa kuimarisha afya ya akili kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia, inayohusiana na ukatili kwa wanawake, wasichana, watoto na makundi mengine ya pembezoni na wale walioathiriwa na vikwazo vya unyanyasaji wa kitamaduni na mijadala katika jamii za vijijini na mijini.

Vilevile alisema unalenga kuhimiza haki na haki za elimu kwa watoto wa kike kwa kuhakikisha kuwa vitendo vya ukatili wa kingono dhidi yao vinatokomezwa na jamii iwe mstari wa mbele kuhimiza na kusaidia wasichana kuingia tena katika mifumo rasmi ya shule.

# Watoto 16,000 wapatiwa msamaha matibabu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

ZAIDI ya watoto 16,000 wenye umri chini ya miaka mitano katika Wilaya ya Hanan'g mkoani Manyara, wamepatiwa msamaha wa matibabu kwa kipindi cha Januari hadi Juni, mwaka huu.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Anna Odimari, alisema hayo jana wakati wa majadiliano ya wadau wa malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ambao wanatekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ( PJT-MMMAM).

Ofisa huyo alisema watoto hao walipatiwa msamaha ili waweze kupata matibabu bure kutokana na kushindwa kumudu gharama za matibabu.

Katika hatua nyingine, alisema kikwazo kikubwa kwa watoto hao ni wazazi kushindwa kuwapeleka kliniki.

Akitoa ufafanuzi juu ya msamaha huo, Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Manyara, Khadija Muwango, alisema katika kutoa msamaha wanaangalia hali ya mzazi kiuchumi na kama mtoto anahudhiria kliniki.

Muwango alisema msamaha wa matibabu siyo unatolewa kwa watoto tu bali ni kwa mujibu wa miongozo ya wizara ambayo inaelekeza kutoa msamaha kwa watoto chini ya miaka mitano,wazee na makundi mengine maalumu.

Naye Mkuu wa Divisheni ya Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii Mkoa wa Manyara, Dk. Damas Kayera, alisema kwa wazazi ambao hawapeleki watoto wao kliniki serikali inatumia Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 ili kuwabana waweze kutekeleza jukumu hilo kwa manufaa ya mtoto na Taifa kwa ujumla.

Alisema kwa mujibu wa sera ya afya ya mwaka 2007, inaeleza kuwa serikali itaboresha na kusimamia sheria,kanuni na miongozo ya uchangiaji gharama za huduma za afya ikiwemo msamaha kwa makundi maalum.

Mkazi wa Kijiji cha Riroda, Rehema Samweli, alisema serikali kutoa msamaha wa matibabu kwa watoto na makundi mengine ni jambo jema ila wazazi nao hata kama familia haina uwezo ni vizuri kusimamia suala la watoto kuhudhuria kliniki ili iwe rahisi serikali kuwasaidia.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Kutoka lingo la miti hadi viwanda vya matofali

**Na Adam Fungamwango**

KWA vijana wa sasa ukimwambia 'lingo la miti' utakuwa umemvuruga. Lakini wa miaka ya 1970 hadi katikati ya 1990 atakuelewa unamaanisha nini.

Kwenye miaka hiyo hasa kwenye jiji la Dar es Salaam na mkoa wa Pwani kulikuwa na maeneo maalum yanayouza miti kwa shughuli mbalimbali za kijamii. Sehemu yoyote wanayouza miti hiyo ndiyo paliitwa 'lingo la miti.'

Kwanza kabisa kulikuwa na miti ile mikubwa kwa ajili ya kujengea nyumba. Ikumbukwe nyumba nyingi za zamani hata za Dar zilikuwa za udongo.

Ila baadaye kukaja teknolojia ya kuzipiga 'lipu', au kuzisakafia kiasi kwamba hata ukipita na kuzitazama huwezi kudhani kuwa ni za udongo.

Nyumba inajengwa kwa udongo halafu kwa nje inapigwa chokaa au saruji na rangi juu, yaani kama siyo mdadisi mpaka ukuta uvunjwe au kubomoka ndiyo utajua kuwa haikuwa ya matofali.

Hata hivyo nyumba hizo mara nyingi zilikuwa ni kubwa kwenye barabara kubwa, ambazo zinawekwa maduka, hoteli, lakini mitaani unakutana na za udongo zenyewe 'laivu'. Wakati huo zilikuwa zinaitwa nyumba za 'mbavu za mbwa.'

Miti ile mikubwa na mirefu ilikuwa inatumika kuchimbia chini kuzunguka eneo litakaloitwa nyumba, halafu itaanza kuzungushiwa fito, yaani miti midogo na miyembamba sana ambazo zinafungwa na kamba kuunganisha ile mikubwa minene mirefu na hii midogo.



**Miti:** Muonekano wa moja ya maeneo yanayouza miti ya kujengea, maarufu kama 'lingo la miti'.



Baada ya hapo katikati yake unakandikwa udongo ambao unakamilisha kuwa nyumba, sasa juu huko ni hiari kama itawekwa bati, nyasi au makuti.

Nyumba nyingi kabla ya kuwekwa paa hazikuwa za staili mbalimbali kama hizi za leo, badala yake zilikuwa na staili moja maarufu kama 'mgongo wa tembo.' Ni kwamba mabati yanaezekwa katikati ya nyumba yalikuwa kama kuna mgongo hivi, halafu kuelekea upande wenye kuta yanashuka chini.

Staili hii iliwekwa ili maji yasituame juu, badala yake mvua ikinyesha yanaserereka na kumwagika chini kwenye ukuta na wanaotaka kukinga maji wanafanya hivyo. Ile miti iliyokuwa inawekwa juu, kabla ya kuezeka mabati na kuitengeneza hiyo staili ya 'mgongo wa tembo' ilikuwa inapatikana kwenye lingo la miti.

Halafu unakutana na fito kama nilivyozitaja hapo nyuma. Kwenye lingo pia unakutana na kuni nene kubwa za kupikia mikate viwandani, lakini pia zipo za kupikia chakula kwenye shughuli mbalimbali za kijamii kama harusi, misiba na nadhalika.

Kunapotokea shughuli hizo, kuna watu hutumwa kwenda lingoni kuchukua kuni kwa ajili ya kupikia chakula.

Hapo nadhani wale ambao hawafahamu 'lingo la miti' angalau sasa wamepata picha.

Kwa miaka ya sasa imekuwa nadra sana kuona 'lingo la miti' au hakuna kabisa hasa mijini kutokana na mabadiliko ya maisha, teknolojia na mengine yanayofanana na hayo.

Hakuna anayejenga nyumba ya udongo kwa sasa sehemu za mijini hivyo biashara ya lingo la miti kukosa soko.

Badala yake watu wanajenga nyumba za matofali ya saruji, hivyo badala ya lingo la miti kuna viwanda vya kufyatulia matofali.

Viwanda vya mikate kwa sasa vinatumia teknolojia ya umeme na si kuni tena, pia kwenye shughuli nyungi za kijamii kwa sasa ama vyakula vinatoka mahotelini, au kwa watu ambao wanachukua tenda ya kupika na kuleta moja kwa moja shughulini, au kuna watu wa kukodi ambao wanakuja kupika hapo hapo, lakini wanakuja na majiko yao ya gesi.

Kwa sababu hii biashara imekufa kifo cha asili. Kwa kupigilia msumari ni kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii imekuwa makini sana na ukataji wa miti, na kwa sheria na kanuni zilizowekwa sasa ukataji miti umepungua sana, hivyo pia kuathiri biashara hiyo.



**Matofali:** Matofali yaliyofyatuliwa yakiwa kiwandani tayari kwa kuuzwa. Hivi ni moja ya viwanda vilivyoua biashara ya kuni na miti ya kujengea.



# Marais SADC wakubali kupeleka jeshi DRC

**LUANDA,** ANGOLA

VIONGOZI wa nchi zinzounda Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Kusini mwa Afrika (SADC), wameridhia kupelekwa kikosi cha kulinda amani Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Kwenye mkutano huo wa Luanda Angola , viongozi hao walipewa taarifa kuhusu hali ya usalama Mashariki mwa DRC na kuidhinisha kutumwa kwa wanajeshi wa nchi za SADC katika jimbo la Kivu.

Taarifa ya pamoja ya mkutano huo ilisema marais wa jumuiya hiyo wamesisitiza kuimarishwa kwa uratibu na uanishaji wa mipango ya amani baina ya pande nne husika ikiwemo jumuiya ya Afrika Mashariki, jumuiya ya nchi za Afrika ya Kati na Kongomano la nchi za Maziwa Makuu (ICGLR).

Viongozi hao walimpongeza pia Rais wa Angola, Joao Lourencou, kwa juhudi zake za upatanishi baina ya DRC na Rwanda ili kutatua mzozo wao kwa njia ya amani.

Hata hivyo haijabainika ni lini na nchi zipi zitatuma wanajeshi wake DRC.

Mwezi Machi , Angola ilitangaza kuchangia wanajeshi mia tano katika kikosi hicho cha SADC wanaopelekwa DRC, lakini ilifahamisha kwamba wanajeshi hao watahusika tu na kusimamia mchakato wa kuwapokonya silaha wapiganaji wa M23.

Namibia pia ilionyesha utayari wake wa kuwapeleka wanajeshi wake.

Mwezi Mei, Rais wa DRC, Felix Tshisekedi, alitishia kuwaondoa wanajeshi wa Afrika mashariki endapo hakutokuwepo na mafanikio yoyote huko Kivu katika kuyasaka makundi ya waasi likiwemo lile la M23.

Wakati huohuo, wanajeshi ya Uganda na DRC wanaopambana na kundi la waasi wa ADF huko Kivu na Ituri walisema waliwaua zaidi ya waasi 548 mnamo kipindi cha miaka miwili ya opereshenі ya pamoja.

Akizuru eneo la Mwalika huko Beni, mkuu wa jeshi la ardhini la Uganda, Lt jenerali Kahanja Muhanga, alisema wamepunguza uwezo wa waasi wa ADF.

**DW**

# Museveni aapa kutopigia magoti Benki ya Dunia

**KAMPALA,** UGANDA

RAIS wa Uganda Yoweri Museveni, ameendelea kuikosoa Benki ya Dunia baada ya kusitisha mikopo kwa nchi yake, akisema taasisi hiyo ya kifedha inajidanganya ikiwa inadhani itawatia hofu wananchi.

Katika taarifa iliyochapishwa kwenye ukurasa wake wa X, ambao zamani ulijulikana Twitter, Rais Museveni aliitaja Benki ya Dunia kama waigizaji wa kibeberu wasio na akili na wasiojua sehemu ya kuacha.

Wiki iliyopita, Benki ya Dunia ilisitisha ufadhili wa kifedha kwa Uganda kwa sababu ya sheria ya kupinga ushoga iliyopitishwa mwezi Mei, ambayo ilikinzana na maadili ya chombo hicho.

Sheria hiyo ambayo imeibua ukosoaji wa kimataifa ya kimagharibi kutokana na adhabu ya kosa hilo ikiwa kifungo au kifo kwa watu wanaojihusisha na vitendo vya jinsia moja.

Wiki iliyopita kiongozi huyo aliishtumu taasisi hiyo kwa kujaribu kuishinikiza Uganda kubadili sheria kwa kusitisha ufadhili, na kuongeza kwamba Uganda itaendelea kujiendesha bila msaada wa Benki ya Dunia.

Jana, Rais Museveni alikaririwa kwamba ufadhili ulioondolewa hautazuia mabadiliko ya kiuchumi ya nchi yake.

Aliongeza kuwa hatua hiyo itasaidia jitihada za Uganda kupunguza deni la nje na kujitegemea zaidi.

Rais Museveni alisema Uganda na washirika wengine kadhaa wa Magharibi ambao wanatishwa, lakini wanaendelea kuiunga mkono Uganda.

**BBC**



Kitongoji cha Wahikuli Terrace kinavyoonekana pichani baada ya moto kuteketeza mali mbalimbali na kusababisha vifo vya watu katika mji wa Lahaina kisiwani Maui katika jimbo la Hawaii, nchini Marekani. **REUTERS**

# Rais Jinping kufanya ziara Afrika Kusini

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa China Xi Jinping anatarajiwa kufanya ziara ya kikazi nchini Afrika Kusini, pamoja na kuhudhuria mkutano wa Brics huko.

Maofisa wa Afrika Kusini wamethibitisha uwepo wa ziara hiyo.

Umoja huo wa Brics unaundwa na nchi za Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini.

Kuundwa kwa umoja huo inaonekana kama mbadala wa kundi la nchi tajiri za G7.

Ziara ya Rais Xi itakuwa ya pili ya kimataifa mwaka huu, baada ya kufanya ziara rasmi nchini Russia mwezi Machi.

Akiwa nchini humo ataungana na viongozi wa mataifa ya Brics yanayotarajiwa kukutana wiki ijayo.

Ajenda kuu ya kikao hicho itakuwa uwezekano wa upanuzi wa jumuiya hiyo kwa kuruhusu kujiunga mataifa mengine.

Nchi kadhaa za Kiafrika, zikiwemo Algeria, Misri na Ethiopia, zimeonyesha nia ya kujiunga na umoja huo.

Awali mkutano huo wa kilele ulikuwa umegubikwa na maswali kuhusu iwapo Rais wa Russia atahudhuria, lakini baadaye na Rais wa Afrika Kusini alithibitisha hatahudhuria.

Rais Putin alikuwa katika mashaka ya kukamatwa na Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kutokana na vita vya Ukraine kama angekwenda Afrika Kusini.

Wakati huo huo, muungano wa vyama saba vya kisiasa nchini Afrika Kusini umetia saini mkataba wa kutaka kukiondoa chama tawala cha African National Congress (ANC) katika uchaguzi wa 2024.

Mkataba huo wa vyama vingi nchini humo ulisema iwapo wataingia madarakani, watafanya kazi pamoja na kugawana nyadhifa za mawaziri na ubunge.

Pia wanalenga kukizuia chama cha Economic Freedom Fighters cha Julius Malema, kupigiwa kura ya kuingia madarakani.

Makubaliano hayo yanakuja wakati nchi hiyo ikikabiliana na hali mbaya ya uchumi, ufisadi, ukosefu wa ajira na mzozo wa nishati.

Wachambuzi wanasema ANC iko hatarini kupoteza wingi wake wa wabunge kwa mara ya kwanza tangu irejee kwenye demokrasia mwaka 1994.

Kambi hiyo mpya, haijaamua ni nani atachaguliwa kuwa rais ikiwa itafaulu katika uchaguzi huo.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHAFI BAKARI ALLY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S0799/0066/2017,** kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia MONDO SECONDARY SCHOOL mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Taarifa polisi: **CHE/RB/655/2023.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**NASIBU SHABANI MNZAVA** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye passport namba: **TAE 137741** iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM PCO mwaka 2019. Lwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIG/1162/2023**

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**ESTHER JAPHET MWINA** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE 382685** iliyotolewa DAR ES SALAAM PCO mwaka 2021 kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DOD/DOD/330/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NOAH ANOSISYE MWAIKUKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye jina la umiliki PAMOJA EXPEDITIONS CO. LIMITED yenye usajili namba **T 937 AER,** CHASSIS NAMBA: **SX410009033** na ENGINE NAMBA: **5S0764930.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAMAL ISSA KIMARO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya NISSAN CARAVAN yenye usajili namba : **T 971 APM** na CHASSIS NAMBA: **CRGE24072381.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/357/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SIGA CLEMENT** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **BOXER BM** yenye usajili namba: **MC 459 DDN**, CHASSIS NAMBA: **MD2B15BX8MWG90769** na ENGINE NAMBA: **JVXWMG66041.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**WMB/RB/1726/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

Ndugu **BARIKI GOODLUCK LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari, lenye namba za usajili **T 398 BZK.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **PHQ/KAG/BUK/3/2023,** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye.

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 23 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE WILLIAM HIZA CHALEMA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTATION**
**BY FRANCIS RICHARD CHALEMA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSON Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the 14th day of the September 2023

Date at Korogwe this 14th day of August 2023

DISTRICT COURT KOROGWE TANZANIA

RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE

RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MWANZA**
**WILAYA YA NYAMAGANA MWANZA**

**SHAURI LA MIRATHI NAMBA 52/2023**

**VICTORIA MRITA..........MSIMAMIZI**

**DHIDI YA**

**OBEDI MRITA........MAREHEMU**

**KUITWA SHAURINI**

MAHAKAMA HII INAKUFAHAMISHA KWAMBA MDAI AMEFUNGUA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU OBEDI MRITA, HATI ZA MIRATHI ZINAPATIKANA KATIKA MAHAKAMA HII.
SHAURI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA MNAMO TAREHE 29/08/2023 SAA 2.00 ASUBUHI NA MNATAKIWA KUWEPO, AU KUWAKILISHWA KISHERIA. YEYOTE MWENYE PINGAMIZI KATIKA MIRATHI HII AHUDHURIE MAHAKAMANI.
ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWENU TAREHE HIYO, SHAURI LITAANZA KUSIKLIZWA BILA NINYI KUTAARIFIWA TENA, NA MAAMUZI KUTOLEWA.
IMETOLEWA KWA MKONO WANGU NA MHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 16/08/2023

HAKIMU MKAZI
WILAYA YA NYAMAGANA
MWANZA

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 80 OF 2023**

**In the Matter of the Estate of the Late: ROSE JOHN NJAU**

**By 1. GOODLUCK JOHN NJAU**
**2. DEOGRATIUS JOHN NJAU**
**3. ROSE JOHN NJAU**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 21 day of 08/2023

**Dated at MOROGORO this 28 day of 07..2023**

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT Morogoro

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KWITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**

**Mahakama ya Mwanzo ya ARUSHA MJINI**
**Wilaya ya ARUSHA**

**MADAI NAMBARI 123 ya 2023**

**Mdai MONICA NTRANSINSIYUS WALINDA**

**Amdai**

**Mdaiwa STANLEY CHARLES KIPALA**
**Kwa STANLEY CHARLES KIPALA**
**Kwa kuwa mdai/ Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba ( Eleza hapa habari za Madai):-**

**UNAAMRIWA NA MAHAKAMA HII UFIKE BILA KUKOSA KUJIBU DAI LA TALAKA MATUNZO YA WATOTO NA MGAWANYO WA MALI**
Kwa hiyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya tarehe 4/09/2023 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angali a kama hukudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu ,Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kwitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakam a hii leo tarehe 15/08/2023
**Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo**


*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake.

## Maiti kwenye kiroba-22

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

***Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani ndio wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Wakinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.***

****************************************




"Hallow mzee Voley habari yako?"

"Nzuri mheshimiwa za huko?"

"Safi, naomba nisaidie kitu kimoja."

"Ndiyo mheshimiwa nakusikia."

"Kati ya yale majina uliyonipa ni nani ambaye ana nyumba kule Ukonga Banana?"

"Charton Antony ndiye mwenye nyumba Ukonga." Halafu akauliza 'Kwani vipi?"

"Hapana, nauliza tu nipate kujua kwa sababu za kikazi."

"Ndiyo hivyo ana nyumba Gongolamboto na nyingine ipo Ukonga Banana, lakini hiyo amempangisha mtu na familia yake."

"Okay, basi nitakutafuta mara nyingine."

"Karibu tena."

Ni mazungumzo ya simu kati ya Eddy na Peter Voley. Huyu ni mjomba wa marehemu Tessy aliyeuawa kikatili kwa kukatwakatwa mapanga na mabaki ya mwili wake kuwekwa kwenye kiroba.

Ni yeye, ndiye awali aliyempa majina ya watu wengi ambayo Eddy Kamal aliyahitaji kwa ajili ya kuanza kufanya upelelezi.

Aliomba majina ya ndugu kadhaa wa marehemu, mashoga zake, na watu wengine ambao aliona anaweza kuanzia upelelezi hapo.

Kitu kilichoanza kumtatiza na kumchanganya hapo ni kuwa, je Charton Antony ndiye aliyekuwepo siku hiyo kwenye nyumba ya Ukonga Banana akawakaribisha Tinga na Mboneka, au ni mpangaji wake kama anavyodai Voley kuwa alimpangisha mtu mweye familia.

"Je huyo mtu aliyepanga nyumba hiyo ni nani? Na kwa nini aliwakaribisha watu hao wawili na kuonekana anamtesa na kumuua mwanamke?" Akajiuliza Eddy.

***************************

Katika kufuatilia kwake akimtumia mtu mmoja dalali wa Banana Ukonga alimletea taarifa kuwa nyumba ile mpaka miezi ambayo mauaji yanatokea haikuwa na mpangaji kwa miezi mitatu.

Taarifa alizozipata ni kwamba mwenye nyumba alimpa notisi mtu aliyepenga nyumba nzima.

Sababu haikupatikana mara moja, lakini mpangaji aliondoka na familia yake na hakuna yoyote aliyeingia.

Cha ajabu ni kwamba baada ya mauaji yale mwezi uliofuata alipatikana mpangaji mwingine anayeishi hadi leo hii.

Hiyo ikampa Eddy Kamal kuhisi kuwa ulikuwa ni mpango maalum uliopangwa kiufundi kabisa.

Aliondolewa mpangaji kwa sababu ya kutekeleza mateso na mauaji ya Tessy kwenye nyumba ile bila kujulikana.

Kwa maana hiyo Charton Antony mwenye nyumba ya Gongolamboto na Ukonga Banana ndiye aliyekuwepo siku ile ya mateso.

Ndiye aliyekuwa na Tinga Patauli kumtesa mwanamke huyo, kumkata viungo akiwa hai na kusababisha kifo chake.

Baada ya hapo wakachukua viungo vyake wanavifunga vizuri wakitumia Mboneka kuubeba.

Kwa nini walimtumia Mboneka na si wao wenyewe?

Ilikuwa ni kama kinga kwao. Chochote kitakachotokea wangeweza kujihami na kukimbia wakimuacha Mboneka ambaye alikuwa hajui chochote.

Ila walikuwa hawajui kuwa Mboneka alikuwa ameshawaona, japo yeye mwenyewe alisema alikuwa hajui amebeba mzigo wa nini.

Charton Antony ni nani? Ni mfanyakazi wa Idara wa Maliasili anayefanya kazi Dodoma.

Tayari ushahidi kwa asilimia 90 unaonyesha kuwa yeye ndiye muuaji wa Tessy.

Eddy alivutiwa na jina lake mwanzoni kabisa alipopewa na mjomba wa marehemu.

Lilikuwa ni moja kati ya majina matano ambayo Eddy alianza nayo katika upelelezi.

Alivutiwa zaidi ya kitendo cha kwenda kwenye semina Mwanza, halafu akawaacha wenzake warudi kazini Dodoma, yeye akasema anabaki kwenye hoteli ya Kangaroo na kwenye hoteli lilionekana jina lake kuwa amelala na mwanamke mmoja.

Ukweli ni kwamba hakulala. Alimtengeneza mtu mwingine kulala na mwanamke akitumia jina lake kwa ajili ya kuficha au kuharibu ushahidi.

Siku ambayo jina lake limeandikwa tena ikionekana amelala kwa siku mbili, alionekana kwenye kamera za CCTV za Uwanja wa Ndege Mwalimu Julius Nyerere akitua na kesho yake akapaa kwenda Dodoma.

Alichokuja kufanya ni kumuua Tessy na kesho yake kurudi Dodoma. Eddy alitumia akili kubwa kufanya upembuzi yakinifu kwani mtekeleza mauaji alitumia akili kubwa.

**Alivutiwa zaidi ya kitendo cha kwenda kwenye semina Mwanza, halafu akawaacha wenzake warudi kazini Dodoma, yeye akasema anabaki kwenye hoteli ya Kangaroo na kwenye hoteli lilionekana jina lake kuwa amelala na mwanamke mmoja.**

Hata kama angekwenda mahakamani angeweza kuruka. Siku ya tukio alikuwa Kangaroo Mwanza na lingeletwa faili la kitabu cha wageni ingeweza kuonyesha kuwa alikuwa huko wakati Tessy akiuawa.

Ushahidi ambao Eddy anao mkononi wa kumtia hatiani ni video ya kamera ya uwanja wa ndege ulionyesha siku hiyo alikuwa Dar es Salaam na alikwenda kutekeleza mauaji Ukonga Banana.

Mashahidi wengine wa dereva taxi, na Mboneka. Kwa nini Charton alionekana kuficha sana mwenendo wake ili isionekane yeye ndiye muuaji.

Yeye ni mume wa Tessy. Ndiyo. Charton ni mume wa Tessy ambapo mpaka anauawa na mumewe akisaidiana na Patauli walikuwa wameishi kwa miaka mitano.

Eddy aligundua mapema kuwa aina ya mauaji hayo mara nyingi hufanywa kwa kisasi na mapenzi na si kitu kingine.

Aina ya mauaji ndiye yaliyofanya kumhisi mumewe tangu mwanzo, ingawa akachukua majina kutoka kwa baadhi ya ndugu wa karibu.

Mauaji ya Tessy aliingia kwenye orodha ya aina ya nne na ya tano ya mauji. Duniani kuna aina ya nane za mauaji.

Mpelelezi yoyote huangalia mauaji yamefanyika vipi na hapo anaweza kuanza kudhani au kuhisi muuaji anaweza kuwa nani.

Aina ya nne ya mauaji ni kwamba muuaji ni kama hawana roho wala hisia, unaweza kusema wenye matatizo ya akili. Huua taratibu na kwa mateso makubwa mno. Hawa ndio wale hutenganisha kiungo kimoja baada ya kingine na wakati mwingine kujirekodi wakati wanafanya hivyo.

Aina ya tano ni wauaji wenye msongo wa mawazo, hufikia kuona kila mmoja ni adui yake hivyo huchukua silaha na kutafuta kadamnasi ya watu na kuwafyatulia risasi, na mara nyingi huishia na kujimaliza na risasi ya mwisho.

Huu ndiyo msingi alioanza nao Eddy. Alijua kabisa muuaji alibebwa mno na hisia, inawezekana ikawa za mapenzi, ndiyo maana alimuua na kukatakata viungo kabla ya kumuua.

Ni mtu anayekupenda zaidi na baadaye kutokea kukuchukia zaidi ndiyo hufanya hivyo hivyo kwa sababu ya hisia. Ni mapenzi ndiyo husababisha mauaji ya aina hiyo.

Ndiyo maana Eddy alishughulika zaidi kufuatilia nyendo za Charton Antony. Na ikawa kama anavyohisi. Mpaka sasa ni yeye tu ndiye aliyekuwa anajua. Hata mjomba wa Tessy hakujua chochote.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

HABARI MICHEZO

# CHAMA AMPA MAJUKUMU MAZITO MIQUISSONE BARA

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Simba, Mzambia Clatous Chama, amemtaka kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Luis Miquissone, ahakikishe anampa pasi za mwisho 10 kwa ajili ya kufunga mabao katika msimu huu mpya ulioanza Agosti 15, mwaka huu.

**Chama ametoa kauli hiyo kufuatia Simba kuibuka na ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Mtibwa Sugar katika mchezo wake wa juzi uliochezwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex ulioko Turiani, Morogoro.**

Katika ushindi wa mchezo huo, Chama alifunga bao la nne baada ya kupokea pasi nzuri kutoka kwa Miquissone ambaye amerejea tena katika timu hiyo akitokea Al Ahly ya Misri.

Akizungumza na Nipashe jana, Chama alisema anaimani kubwa atafanya vyema na vizuri msimu huu kwa kufunga mabao kutokana na muunganiko mzuri wa wachezaji wenzake hasa Miquissone ambaye aliwahi kucheza naye miaka ya nyuma.

Chama alisema anafurahi Simba kupata ushindi wa mabao 4-2, huku yeye pia akifunga katika ushindi huo wa kwanza msimu huu.

"Nimefurahi kupata pasi ya mwisho na kufunga kutoka kwa Miquissone (Luis), ila nataka assist 10 kutoka kwa nyota huyo katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema kiungo huyo.

Aliongeza kwa ubora wa kikosi chao, anaimani wanatarajia watafanya vizuri zaidi ya msimu uliopita na hiyo inatokana na maboresho yaliyofanyika kwa kusajili wachezaji wapya ambao wamekuja kusaidia kufikia malengo ya kutwaa mataji mbalimbali yaliyopo mbele yao.

Mabao mengine ya Simba katika mechi hiyo yalifungwa na Jean Baleke, Essomba Onana na Fabrice Ngoma.

Tayari Simba imeanza vyema msimu kwa kubeba Ngao ya Jamii iliyokuwa inashikiliwa na watani zao, Yanga.




## Namungo hasira kwa KMC FC

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kupoteza mechi ya kwanza, Namungo FC inatarajia kuwakaribisha KMC katika mchezo wa raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, mkoani Lindi.

Kocha Mkuu wa Namungo, Cedric Kaze, aliliambia gazeti hili hana wasiwasi wowote kuelekea mchezo huo na anaamini wachezaji wake watacheza kwa tahadhari ili kuzibakisha pointi tatu nyumbani.



Kaze (pichani) alisema anafahamu mechi hiyo itakuwa na ushindani mkubwa kutokana na ubora wa wachezaji wa KMC, lakini amekifanyia maboresho kikosi chake.

"Nitaingia uwanjani nikiwa na tahadhari kwa sababu timu zote zimefanya usajili mzuri, makosa niliyoyaona katika mchezo uliopita dhidi ya JKT Tanzania nimeyafanyia kazi, hayawezi kujirudia," alisema Kaze.

Aliongeza kila mchezaji wake sasa ana shauku ya kufanya vizuri kutokana na ushindani waliouonyesha mazoezini.

Naye Katibu Mkuu wa timu hiyo, Ally Mkadeba, alisema malengo yao ni kuhakikisha hawaupotezi mchezo huo wa pili.

Mechi nyingine ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Ihefu dhidi ya Kagera Sugar.




Wachezaji wa Azam FC wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji Bahir Dar Kenema utakaochezwa kesho nchini Ethiopia. **PICHA: MTANDAO**

## Mashujaa FC yajipanga kuimaliza Geita Gold

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mashujaa FC, Abdallah Mohammed 'Bares', amesema ataingia na mfumo mwingine wa kuongeza idadi ya washambuliaji katika mechi yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold FC itakayochezwa kesho kutwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Bares alisema licha ya kupata ushindi katika mechi yao ya kwanza, ameyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza ili kuwa na kikosi imara zaidi.

Kocha huyo alisema katika mechi ijayo ataingia tofauti ili kuwachanganya wapinzani wao na kwa sababu anafahamu mbinu za Kocha wa Geita Gold FC, Hemed Morocco, ambaye ni Mzanzibar mwenzake.

"Hii mechi yetu itakuwa ya ushindani mkubwa, naamini mbinu zitatawala zaidi katika mchezo, makocha wote tunatoka sehemu moja na kila mmoja wetu anafahamu ubora wa mwenzake.

Utakuwa mchezo mzuri, ninategemea kufanya mabadiliko ya kikosi lakini pia kuongeza watu mbele kulingana na ubora wa wapinzani wetu katika kila eneo, tunahitaji kushinda mechi hiyo," alisema Bares.

## JKT Queens, Vihiga majaribuni CECAFA Uganda

**Na Abdallah Mataka**

WAWAKILISHI wa Tanzania Bara, JKT Queens wanakutana na Vihiga Queens katika mechi ya mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati itakayofanyika kwenye Uwanja wa Lugogo jijini Kampala, Uganda.

JKT Queens yenye pointi sita tayari imeshatinga hatua ya nusu fainali baada ya kushinda mechi zake mbili ilizocheza dhidi ya AS Kigali ya Rwanda na New Generation ya Zanzibar.

Ofisa Habari wa JKT Queens, Masau Bwire, alisema wachezaji wote wako tayari kuelekea mchezo huo na wamejipanga kuendelea kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.

"Ni mchezo ambao tunahitaji kupata matokeo chanya bila kuangalia kundi limekaaje, lengo letu sisi ni kuonyesha ubora wetu katika haya mashindano, kwa uwezo wa Mungu tunataka tuchukue ubingwa wa mashindano haya ikiwa hatujapoteza mchezo wowote," alisema Bwire.

Alisema JKT Queens inataka kurejea nyumbani na ubingwa wa mashindano hayo ambayo mwaka jana ulichukuliwa na Simba Queens ya Dar es Salaam.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE ATOA MSIMAMO

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 24, amewaambia wawakilishi wake kuwa atabakia PSG mwaka huu lakini mwaka 2024 anataka kuchezea Real Madrid. ***(El Chiringuito TV)***

### JOHNSON ANUKIA CHELSEA

CHELSEA wamemwongeza mshambuliaji wa Nottingham Forest na Wales, Brennan Johnson, 22, kwenye orodha ya washambuliaji na wamefanya mazungumzo ya awali na mchezaji huyo. ***(Guardian)***

### SPURS, FOREST VITANI

KLABU ya Nottingham Forest imeweka dau la pauni milioni 40 kwa Brennan Johnson, huku Tottenham na Brentford pia zikifikiria kumnunua mshambuliaji huyo kabla ya dirisha la usajili kufungwa. ***(Independent)***

### DOKU ATAJWA CHELSEA

CHELSEA wameulizia kuhusu winga wa Rennes na Ubelgiji, Jeremy Doku, 21, baada ya uhamisho wao wa kumnunua Michael Olise wa Crystal Palace kushindikana. ***(90 Min)***

### BARCOLA AGOMBEWA ULAYA

CHELSEA pia inamtazama winga Mfaransa, Bradley Barcola, 20, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Paris St-Germain ambao wamelazimika kutoa ofa ya euro milioni 35 na klabu yake ya Lyon. ***(RMC Sport)***

### MONACO KUMUUZA SANCHEZ

DAVINSON Sanchez, 27, analengwa na Monaco baada ya Tottenham Hotspur kumweka sokoni mlinzi huyo wa Timu ya Taifa ya Colombia. ***(Telegraph)***

### CITY YAMWANIA BARCO

KLABU ya Manchester City inajaribu kuipiku Brighton katika kumsajili beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Argentina Valentin Barco, 19, kutoka Boca Juniors. ***(Mail)***

### BAYERN YAMKATAA DE GEA

BAYERN Munich haitamsajili mlinda mlango wa Hispania, David de Gea, 32, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Manchester United, huku kocha, Thomas Tuchel akipinga wazo hilo. ***(Florian Plettenberg)***

### PAVARD NJIA PANDA

BEKI wa Bayern Munich, Benjamin Pavard, 27, anatazamiwa kuchagua kati ya kuhamia Manchester United au Inter Milan kabla ya mwisho wa dirisha. ***(L'Equipe)***

### ENDO KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL iko tayari kukamilisha usajili wa Wataru Endo, 30, huku Stuttgart ikiwa imekubali dau la pauni milioni 16 kwa kiungo huyo wa kati wa Japan. ***(Football Insider)***

### WEST HAM SOKONI

KLABU ya West Ham inakaribia kuafikiana na Stuttgart kwa ajili ya kumnunua beki wa Ugiriki, Konstantinos Mavropanos, 25. ***(Sky Sports, via Football Daily)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KANE AFUNGUKA SIRI ILIYOMPELEKA BAYERN

**MUNICH,** Ujerumani

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya England na nyota wa zamani wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, amefichua aliamua kujiunga na Bayern Munich ili kushinda mataji.

**Licha ya kufunga mabao 354 katika maisha yake ya soka hadi sasa, na kushinda tuzo kadhaa binafsi, Kane bado hajashinda hata taji la timu moja katika maisha yake ya soka.**

Mwaka 2019 alikaribia kutwaa taji wakati Spurs ilipocheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini wakafungwa na Liverpool na pia kwenye euro 2020 alitinga fainali na England na walipoteza kwa penalti dhidi ya Italia.

Akizungumza na Sky Sports News kwa mara ya kwanza tangu auzwe kwa kitita cha pauni milioni 86 kutoka Tottenham kwenda Bayern, Kane alikiri kutaka kushinda medali ndiyo sababu kubwa ya kuhamia kwa miamba hao wa Bavaria.

## ●●● Mshambuliaji huyo asema ni kiu ya kushinda mataji na kupata...

"Watu wengi huzungumza juu ya mataji na kwa nini nilikuja hapa, lakini hatimaye ilikuwa kuboresha, kuhisi shinikizo mpya la kushinda mataji kila mwaka, kulazimika kufika mbali kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kujisukuma kufikia kikomo hicho, " alisema.

"Ikiwa unashinda michezo, ikiwa unashinda mataji ya Ligi ya Mabingwa na mimi ndiye ninacheza mbele, kuna uwezekano mkubwa mimi ndiye ninayefunga mabao, ambayo hukuruhusu kushinda.

"Tuna msimu mrefu mbele. Kuna shinikizo kubwa kwa Bayern Munich kushinda ligi na kufika mbali katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, na hilo ndilo ninalofurahia kujipa changamoto. Unapokuwa kwenye klabu kama Bayern Munich lazima ushinde. Hakuna maswali kuihusu.

"Ni ngumu kuweka namba juu ya mataji mangapi unataka kushinda lakini siku zote nimekuwa nikisema katika maisha yangu yote sitaki kustaafu na kuhisi kama ningeweza kufanya zaidi au ningeweza kujisukuma zaidi.

"Hiyo ilikuwa sehemu kubwa ya mchakato wa kufanya uamuzi wa kuja Bayern Munich kwa sababu ili kuimarika na kuwa bora ilinibidi kucheza katika kiwango cha juu zaidi.

"Bila shaka, nataka kushinda kila shindano ninalocheza. Hilo ndilo lengo kuu kila msimu, lakini unapomaliza kazi yako, wakati wowote, unataka tu kuhakikisha umejiweka kwenye kikomo chako."

Kane anatarajiwa kucheza mechi yake ya kwanza ya Bundesliga wikendi hii wakati Bayern Munich watakapomenyana na Werder Bremen.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,144,1

MECHI KALI
TOTTENHAM
VERSUS
MANCHESTER UNITED
1 | 2.72
X | 3.57
2 | 2.48

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MESSI, DE BRUYNE NA HAALAND WAWANIA TUZO

**LONDON,** England

LIONEL Messi ameingia kwenye orodha ya wachezaji watatu waliotangazwa kuwania tuzo ya UEFA kama mchezaji bora wa Ulaya msimu uliopita.

Nahodha huyo aliyeshinda Kombe la Dunia akiwa na Argentina, ambaye ameondoka Ulaya na kujiunga na Inter Miami CF ya Marekani, anachuana na wachezaji wa Manchester City, Kevin De Bruyne na Erling Haaland.

Messi alishinda tuzo ya UEFA mara mbili katika historia yake ya miaka 12, katika miaka ambayo Barcelona walikuwa Mabingwa wa Ulaya. Manchester City ilishinda taji la Ligi ya Mabingwa msimu uliopita.

Pep Guardiola ndiye anayepewa nafasi kubwa ya kutwaa tuzo ya ukocha bora kwa wanaume baada ya kuiongoza City kutwaa mataji ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu na Kombe la FA.

Makocha wengine ni Simone Inzaghi wa Inter Milan, ambaye aliiongoza timu yake kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na Luciano Spalletti, aliyeiongoza Napoli kutwaa taji la Ligi Kuu Italia.

Washindi watatangazwa kwenye droo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Agosti 31, mwaka huu huko Monaco.

Orodha fupi za tuzo za mchezaji na kocha wa wanawake zitatangazwa wiki ijayo baada ya kumalizika kwa fainali za Kombe la Dunia la Wanawake, UEFA ilisema.



## Walcott atangaza kustaafu soka

**LONDON,** England

WINGA wa zamani wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England, Theo Walcott ametangaza kustaafu soka akiwa na umri wa miaka 34, baada ya kukataa ofa kutoka Saudi Arabia.

Walcott alichezea klabu yake ya utotoni ya Southampton, lakini aliachwa mwishoni mwa msimu uliopita.

Alipata umaarufu akiwa na Southampton akiwa na umri wa miaka 16, kabla ya kujiunga na Arsenal na kuitwa kwenye kikosi cha England kwenye fainali za Kombe la Dunia la mwaka 2006 ndani ya miezi miwili baada ya kufikisha miaka 17.

Wakati huo, Walcott alikuwa bado hajacheza mechi yake ya kwanza ya wakubwa Arsenal, lakini aliendelea kucheza mechi 400 tu akiwa na washikabunduki katika kipindi cha miaka 12 - akifunga mabao 108 na kushinda mataji mawili ya FA.

Huku maisha ya soka ya Arsenal yakizidi kuzorota, fowadi huyo alijiunga na Everton kwa pauni milioni 20 Januari 2018. Mkopo wa 2020 kwa Southampton ulifuatiwa na uhamisho wa kudumu mwaka uliofuata.

## HABARI MICHEZO

72,464/-

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/08/23 | 17:00 | Fulham FC vs Brentford FC | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 02. 19/08/23 | 19:15 | Caykur Rizespor vs Alanyaspor | 2.36 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 19/08/23 | 19:30 | Tottenham Hotspur vs Manchester United | 3.00 | 3.40 | 2.21 |
| 04. 19/08/23 | 19:30 | Empoli FC vs Hellas Verona | 2.35 | 3.15 | 2.95 |
| 05. 19/08/23 | 21:45 | Hatayspor Antakya vs Kasimpasa Istanbul | 2.32 | 3.35 | 2.60 |
| 06. 19/08/23 | 21:45 | Genoa CFC vs ACF Fiorentina | 2.95 | 3.25 | 2.30 |
| 07. 19/08/23 | 22:30 | Portimonense SC vs Boavista Porto | 2.43 | 3.10 | 2.90 |
| 08. 19/08/23 | 22:30 | CA Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.75 | 3.05 | 2.60 |
| 09. 20/08/23 | 14:30 | VfL 1899 Osnabruck vs FC Nuremberg | 2.48 | 3.40 | 2.60 |
| 10. 20/08/23 | 14:30 | Holstein Kiel vs FC Magdeburg | 2.35 | 3.55 | 2.70 |
| 11. 20/08/23 | 16:00 | Le Havre AC vs Stade Brest 29 | 2.55 | 3.20 | 2.65 |
| 12. 20/08/23 | 16:00 | FC Lorient vs OGC Nice | 3.05 | 3.40 | 2.18 |
| 13. 20/08/23 | 17:30 | Estoril Praia vs Rio Ave FC | 2.40 | 3.15 | 2.90 |
| 14. 20/08/23 | 18:00 | Hamarkameratene vs Rosenborg BK | 2.70 | 3.25 | 2.26 |
| 15. 20/08/23 | 19:00 | FC Sudtirol Bolzano vs Spezia Calcio | 3.15 | 2.95 | 2.15 |
| 16. 20/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs KAS Eupen | 2.15 | 3.45 | 3.10 |
| 17. 20/08/23 | 21:45 | RC Lens vs Stade Rennes | 2.33 | 3.50 | 2.75 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 19/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:00 | 2224 | Sweden W vs Australia W | 2.39 | 3.27 | 2.66 |
| 15:00 | 5057 | Dinamo Moscow vs CSKA Moscow | 2.62 | 3.44 | 2.39 |
| 16:00 | 1285 | Nkana FC vs Red Arrows | 2.65 | 2.60 | 2.80 |
| 16:00 | 1849 | Ihefu FC vs Kagera Sugar | 1.79 | 3.15 | 5.00 |
| 16:00 | 4007 | Polokwane City vs Ajax Cape Town | 2.23 | 2.89 | 3.40 |
| 16:30 | 1847 | Augsburg vs Monchengladbach | 2.72 | 3.60 | 2.47 |
| 16:30 | 2750 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.46 | 3.54 | 2.77 |
| 16:30 | 3265 | Stuttgart vs VfL Bochum | 1.70 | 4.13 | 4.54 |
| 16:30 | 3864 | Al Hikma vs Safa SC | 2.70 | 2.95 | 2.43 |
| 16:30 | 4629 | VfL Wolfsburg vs Heidenheim | 1.63 | 4.21 | 5.03 |
| 16:30 | 5044 | Hoffenheim vs SC Freiburg | 2.29 | 3.60 | 2.99 |
| 17:00 | 2976 | Liverpool vs Bournemouth | 1.29 | 5.93 | 9.26 |
| 17:00 | 3968 | QPR vs Ipswich | 3.67 | 3.37 | 1.92 |
| 17:00 | 3993 | Middlesbrough vs Huddersfield | 1.66 | 3.67 | 4.66 |
| 17:00 | 4902 | Sheffield Wed vs Preston | 2.45 | 3.11 | 2.77 |
| 17:00 | 5323 | Bristol City vs Birmingham | 2.00 | 3.42 | 3.37 |
| 17:00 | 5777 | Leicester vs Cardiff | 1.52 | 3.93 | 5.63 |
| 17:00 | 5836 | Fulham vs Brentford | 2.58 | 3.36 | 2.74 |
| 17:00 | 5964 | Blackburn vs Hull City | 1.88 | 3.47 | 3.72 |
| 17:30 | 5256 | SBV Excelsior vs Ajax | 9.10 | 6.33 | 1.22 |
| 18:00 | 1863 | Bkma Yerevan vs Alashkert Martuni | 3.71 | 3.31 | 1.89 |
| 18:00 | 1945 | Aksu vs Atyrau | 2.49 | 2.98 | 2.68 |
| 18:00 | 4164 | Real Sociedad vs Celta Vigo | 1.78 | 3.45 | 5.04 |
| 18:00 | 4777 | Austria Lustenau vs Sturm Graz | 5.26 | 4.05 | 1.49 |
| 18:30 | 3313 | Amazulu vs Richards Bay FC | 2.02 | 2.98 | 3.86 |
| 19:00 | 3612 | Molde vs Valerenga | 1.37 | 4.75 | 6.82 |
| 19:15 | 1806 | Barry Town FC vs Colwyn Bay | 2.24 | 3.37 | 2.72 |
| 19:30 | 2205 | Tottenham vs Manchester Utd | 2.72 | 3.57 | 2.48 |
| 19:30 | 2879 | Empoli vs Verona | 2.34 | 3.29 | 3.13 |
| 19:30 | 4270 | Frosinone vs Napoli | 8.03 | 4.78 | 1.40 |
| 19:30 | 4603 | Borussia Dortmund vs FC Koln | 1.42 | 5.15 | 6.59 |
| 19:45 | 4596 | Vitesse Arnhem vs PSV Eindhoven | 4.26 | 4.26 | 1.61 |
| 20:00 | 1313 | GD Chaves vs Sporting Braga | 5.38 | 3.74 | 1.58 |
| 20:00 | 2179 | Sochi vs Rostov | 2.32 | 3.23 | 2.87 |
| 20:00 | 2714 | Vojvodina vs Radnicki Nis | 1.54 | 3.68 | 5.25 |
| 20:00 | 5783 | Lyon vs Montpellier | 1.66 | 4.21 | 4.73 |
| 20:30 | 3472 | Almeria vs Real Madrid | 6.71 | 4.61 | 1.46 |
| 21:00 | 3155 | Al Hilal Riyadh vs AL Faiha | 1.42 | 4.19 | 7.75 |
| 21:00 | 4532 | Paksi FC vs Ujpest FC | 2.23 | 3.47 | 2.75 |
| 21:30 | 3648 | Red Star Belgrade vs Spartak Subotica | 1.04 | 9.13 | 23.32 |
| 21:45 | 1966 | Inter vs Monza | 1.45 | 4.69 | 6.89 |
| 21:45 | 2195 | Genoa vs Fiorentina | 3.29 | 3.29 | 2.26 |
| 21:45 | 3032 | AEK Athens vs Dinamo Zagreb | 2.12 | 3.12 | 3.37 |
| 21:45 | 4286 | Galatasaray vs Trabzonspor | 1.64 | 3.93 | 4.52 |
| 21:45 | 5379 | Mechelen vs Union Saint Gilloise | 4.27 | 3.77 | 1.71 |
| 22:00 | 1585 | Sao Paulo vs Botafogo RJ | 1.99 | 3.28 | 3.43 |
| 22:00 | 1702 | Toulouse vs Paris St Germain | 4.60 | 4.01 | 1.71 |
| 22:00 | 3938 | Manchester City vs Newcastle | 1.77 | 3.84 | 4.43 |
| 22:30 | 4129 | Osasuna vs Athletic Bilbao | 2.81 | 3.07 | 2.71 |
| 22:30 | 4235 | Benfica vs CF Estrela | 1.16 | 6.77 | 13.94 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MTIBWA SUGAR YAANIKA SABABU ILIYOWAANGUSHA

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Habib Kondo, ameitupia lawama safu ya ulinzi ya timu yake kwa kukosa umakini na kusababisha kupokea kichapo cha mabao 4-2 kutoka kwa Simba walipokutana katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro juzi.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Kondo alisema safu yake ya ulinzi ilipoteza utulivu na kushindwa kulinda mabao mawili ya kusawazisha aliyofunga Matheo Anthony (pichani) baada ya Simba kutangulia kufunga magoli hayo.

**Kondo alisema mabeki wake walishindwa kuwabana washambuliaji wa Simba ambao walitegemea zaidi safu ya viungo.**

"Safu ya ulinzi haikuwa makini, tulipata nafasi nyingi tukashindwa kuzitumia na badala yake Simba wakapata mwanya wa kutufunga kirahisi," alisema Kondo.

Kocha huyo alisema licha ya kupoteza mchezo huo bado hajakata tamaa kwa sababu bado ni mapema.

"Tunaahidi tunajipanga upya kwa ajili ya mchezo ujao, tutawakabili Coastal Union kwa tahadhari, tunayafanyia kazi makosa yote yaliyojitokeza tulipocheza dhidi ya Simba," Kondo alisema.

Hata hivyo aliongeza wachezaji wake walionyesha uwezo mzuri katika mechi hiyo na kuwataka waongeze juhudi watakapokutana na Coastal Union.

Aliwataka mashabiki wao wajitokeze kwa wingi katika mechi ya kesho ili kuwapa morali na hatimaye watimize malengo.





Kikosi cha KMKM FC ya Zanzibar kilichoanza katika mechi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya St. George kutoka Ethiopia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana. KMKM ilifungwa mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yaliota 'pira, biriani'

ENDELEA UKURASA 23

haya," alisema.

Kuhusu ushindi walioupata Ahmed alisema ulikuwa muhimu mno kwa sababu nyingi, ikiwamo kuendeleza furaha ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo walioanza kuipata kuanzia katika Tamasha la Simba Day na Jumapili iliyopita walipobeba Ngao ya Jamii.

"Mara nyingi mechi za kwanza huwa hivyo, Mtibwa Sugar ilikuwa na wachezaji vijana wenye nguvu wanaokimbia muda wote na wanakaba, hii ilitupa tabu kidogo, ila ukomavu wa wachezaji wetu umetusaidia," alisema ofisa hiyo.

Kwa ushindi huo Simba iko katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara nyuma ya Azam FC inayoongoza ligi hiyo baada ya kuitandika Kitayosce mabao 4-0.

## *Gamondi : Nahitaji mabao mengi CAF*

ENDELEA UKURASA 23

katika msimu uliopita.

"Kikosi kimeshaingia kambini, kocha wetu anaendelea na maandalizi yake ikiwamo kuiongezea makali safu ya ushambuliaji ili kuhakikisha wanafikia malengo ya kuvuka katika hatua hii ya kwanza," alisema Kamwe.

Msimu uliopita Yanga ilipoteza mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya matokeo ya jumla kuwa sare ya mabao 2-2, ikikubali kufungwa nyumbani na mabingwa USM Alger ya Algeria magoli 2-1 na kushinda ugenini bao 1-0.

Yanga, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara iliangukia katika michuano hiyo baada ya kutolewa katika Ligi ya Mabingwa Afrika na Al Hilal ya Sudan kwa kufungwa jumla ya mabao 2-1.

Michezo
Jumamosi Agosti 19, 2023
Nipashe



Walcott atangaza kustaafu UKURASA 22



Straika wa Yanga, Stephano Aziz Ki (kulia), akijiandaa kuondoka na mpira katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kuivaa ASAS FC kutoka Djibouti kuelekea mechi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# GAMONDI: NAHITAJI MABAO MENGI CAF

## ●●● Musonda, Mzize watakiwa kuongoza mashambulizi katika mechi hiyo ili...

**Na Saada Akida**

ILI kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema anahitaji kuona safu yake ya ushambuliaji inakuwa 'moto' katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Al Sabieh (Asas FC) kutoka Djibouti ili kurahisisha kazi.

**Yanga watakuwa ugenini katika mchezo huo utakaofanyika kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na marudiano wiki ijayo kutokana na Wadjibouti hao kutumia uwanja huo huo.**

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi, alisema amewapa washambuliaji wake mazoezi maalumu kwa sababu anataka kuona wanafunga mabao mengi na kumaliza 'kibarua' katika mchezo huo wa kwanza.

Kocha huyo alisema endapo watapata ushindi mnono katika mechi ya kesho, watakuwa wamerahisisha kazi kuelekea mchezo wa marudiano na wamejiandaa kukutana na ushindani kutoka kwa wapinzani wao.

Alisema katika mazoezi amekuwa akipambana kuhakikisha safu yake ya ushambuliaji inayoongozwa na Kennedy Musonda na Clement Mzize kuongeza utulivu baada ya kushindwa kuonyesha makali yake katika fainali ya Ngao ya Jamii iliyochezwa Jumapili iliyopita.

"Tungependa kuanza vizuri mashindano haya ya CAF, ukipata ushindi katika mechi ya kwanza, kazi inakuwa nyepesi kuelekea mchezo unaofuata wa marudiano, siku hizi hakuna timu ndogo, soka limebadilika, tunahitaji ushindi katika kila mechi," Gamondi alisema.

Aliongeza anatarajia pia kutumia washambuliaji wengi katika mechi ya kesho ili wafikie malengo ya kupata ushindi mnono.

"Tutaingia uwanjani kwa kushambulia sana wapinzani wetu ili kuhakikisha tunapata mabao ya mapema, tunataka ushindi mkubwa katika mchezo wa kwanza, hatutawadharau pia wapinzani wetu," Gamondi alisema.

Alisema anafurahi kuona kila mchezaji anapambana kuhakikisha anapata namba katika kikosi cha kwanza kwa kuonyesha uwezo mkubwa mazoezini na hali hiyo inasaidia kuimarisha kikosi.

Kocha huyo alisema anaimani na kikosi chake kitafanya vizuri katika mchezo huo ambao utatoa mwanga klabu yao katika michuano hiyo ya kimataifa.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema maandalizi yote muhimu kuelekea mechi hiyo yamekamilika na wageni wao wamewasili mapema.

Kamwe alisema kikosi cha Yanga kimejiandaa kuendelea kuwapa furaha mashabiki wake furaha kama ilivyofanya

ENDELEA UKURASA 23

# Simba SC yaliota 'pira, soka biriani'

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuvuna pointi tatu ugenini kwa kuichapa Mtibwa Sugar mabao 4-2, Simba imekiri kwa sasa kikosi chao kimekuwa hakichezi soka la kuvutia maarufu 'pira biriani' kama ambavyo mashabiki wake wamezoea na hiyo inatokana na maingizo ya wachezaji wengi wapya, imeelezwa.

Hata hivyo baadhi ya mashabiki wa timu hiyo na wachambuzi wa soka nchini wameonyesha mashaka juu ya kiwango kilichoonyesha katika mechi hiyo ya juzi kwa kuruhusu mabao mawili ya haraka kizembe.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kwa sasa wao wanahitaji zaidi ushindi na anaamini soka la burudani litaanza kuonekana ndani ya mechi chache zinazokuja.

Ahmed alisema suala la kucheza mpira wa kuvutia siyo la siku moja au baada ya kutoka kwenye 'pre season', badala yake linahitaji muda na amewataka mashabiki wa timu hiyo kuwa na subira kwa sababu burudani wanayoitaka itarejea baada ya kikosi kupata muunganiko.

"Bado watu hawajaridhika kwa sababu hawajaiona ile Simba yao wanayoitaka na waliyoizoea ya mpira wa burudani, mpira mwingi au wenyewe wanauita 'pira biriani', lakini ni lazima watambue hizi ni mechi za kwanza, bado timu inajitafuta, kwa sasa tunacheza tupate matokeo huku makocha wakiitengeneza timu itakayocheza vizuri baadaye, wawe na subira," alisema Ahmed.

Aliongeza mabao mawili waliyoruhusu hayakuwa makosa ya kimfumo, badala yake yalikuwa ni ya mchezaji mmoja mmoja, huku akiamini Kocha Mkuu, Roberto Oliveira atayatatua.

"Yapo makosa mengi ambayo yametokea kwenye mchezo wetu yaliyozaa mabao mawili katika mechi ya leo, ukiangalia mengi yanatokana na makosa binafsi ya wachezaji wetu, ni kitu cha kawaida kwenye mpira wa miguu, mwalimu anakwenda kuangalia wapi kwa kuboresha ili mechi zinazofuata tusirudie makosa kama

ENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >